

**HAJA YA LUGHA YA KISWAHILI KUTUMIKA KUFUNDISHIA ELIMU
YA SEKONDARI: MIFANO KUTOKA WILAYA YA ILEMELA-MWANZA**

NICHOLAUS MVUGAMAKE LUNYANA

**TASNIFU INAWASILISHWA KATIKA KUKAMILISHA MASHARTI
YANAYOTAKIWA KWA AJILI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO
KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2015

UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa amesoma tasnifu hii itwayo”**Haja ya lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia elimu ya Sekondari**” na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya shahada ya uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

.....
Dk.Nestory Ligembe

(Msimamizi)

.....
Tarehe

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa baadhi ya maandishi ya kitabu hiki, kwa namna yoyote ile bila ya idhini ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi **Nicholaus Mvugamake Lunyana** natamka na nathibitisha kwa seneti ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwamba tasnifu hii kwa ajili ya shahada ya uzamili ya Kiswahili ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa pahali pengine kwa lengo la kunukiwa shahada ya aina hii.

.....
Sahihi

.....
Tarehe

TABARUKU

Tasnifu hii namtabaruki mama yangu mzazi Bi.Deborah Kenguye aliyenilea na kunifanya niwe na kiu ya masomo ili niweze kufaulu maishani.Namtabaruku kaka yangu Erasto na Dada yangu Jesca Mvugamake ambao walitoa michango yao mbalimbali kuwezesha masomo yangu nilipokuwa bado ni tegemezi.Daima nitakumbuka yote mliyonifanya kwa ajili ya maisha yangu.

SHUKURANI

Kazi ya utafiti huu isingeweza kukamilika bila ya msaada wa watu mbalimbali. Juhudi na michango ya hali na mali yaa watu hao ilisaidia kukamilisha kazi ya utafiti huu. Hivyo basi, natumia nafasi hii kuwataja baadhi yao ili kuwakilisha wengine ambao sitawataja. Wale ambao hawataweza kutajwa. Siyo kwamba sikuwakumbuka bali natambua na kuthamini umuhimu wao na mawazo ya kila mmoja ambayo kwa kiasi kikubwa yamewezesha tasnifu hii kikamilifu. Hivyo nawashukuru sana. Kwanza, namshukru Mwenyezi Mungu aliyenipa afya mimi mwenyewe pamoja na familia yangu tangu nilipoanza masomo ya kiwango hiki cha shahada ya uzamili. Aidha, neema yake ilikuwa juu yangu na kunipa uwezo na nguvu ya kukamilisha kazi ya utafiti huu. Pili, shukrani zangu za dhati zimwendee msimamizi wangu Dk. Nestory Ligembe wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Uzoefu wake binafsi, uvumilivu, upendo na ujuzi wake wa kazi za utafiti na ushauri wake umesaidia sana kukamilika kwa tasnifu hii. Tatu, kwa moyo mweupe napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wahadhiri wote waliotumia muda wao kunifundisha wakati wa mihadhra ya darasani ambao ni: Prof. Sengo, T.S.Y.M, Prof. James S. Mdee, Dk. Zelda Elisifa, Dk. Hanna Simpassa na Dk. Pembe Lipembe wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa jinsi walivyo jitoa wakati wote kunifundisha, kuendeleza na kukamilisha maarifa na stadi zilizohitajiwa ili kumilisha kiwango cha shahada hii.

IKISIRI

Utafiti huu ulikusudia kuchunguza haja ya lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia elimu ya sekondari kwa kutumia mifano kutoka Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza uhusiano baina ya kutotumika kwa Kiswahili katika ufundishaji wa masomo katika shule za sekondari na kushindwa kwa wanafunzi kupata maarifa yaliyokusudiwa. Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi ambayo ni; Kubainisha mambo yanayo changia wanafunzi kukosa maarifa ya elimu ya sekondari, kubainisha athari zitokanazo na kutotumika kwa lugha ya Kiswahili katika kufundishia elimu ya sekondari na kujadili changamoto zinazowakabili walimu na wanafunzi zitokanazo na kutotumika kwa Kiswahili katika ufundishaji wa elimu ya sekondari. Ili kufikia malengo hayo, utafiti huu ulitumia mbinu za maktaba, hojaji na dodoso. Nadharia iliyotumika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu ni nadharia ya Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kuwa, walimu na wanafunzi wanapendelea elimu ya sekondari itolewe kwa lugha ya Kiswahili badala ya kutumia lugha ya kigeni. Utafiti umedhihirisha kuwa, utolewaji wa elimu ya sekondari kwa lugha ya kigeni hauna mafanikio makubwa hata kama kauli mbiu ya sasa ya serikali ni matokeo makubwa sasa. Ni vigumu kupata matokeo makubwa ikiwa wanafunzi hawaelewa wanachofundishwa. Ili kupata matokeo makubwa na yenye ufanisi ni lazima serikali na wadau wote wa elimu waamue kukifanya kiswahili kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari.

YALIYOMO

UTHIBITISHO	ii
HAKIMILIKI	iii
TAMKO LA MTAHINIWA	iv
TABARUKU	v
SHUKURANI	vi
IKISIRI	vii
YALIYOMO	viii
SURA YA KWANZA	1
1.0 UTANGULIZI WA JUMLA	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Usuli wa Tatizo	1
1.3 Tatizo la Utafiti	8
1.4 Malengo ya Utafiti	9
1.4.1 Lengo Kuu.....	9
1.4.2 Malengo mahususi ya utafiti	9
1.5 Maswali ya Utafiti	9
1.6 Umuhimu wa Utafiti.....	10
1.6.1 Wanataaluma	10
1.6.2 Watunga Sera ya elimu	10
1.6.3 Jamii ya Watanzania.....	11
1.6.4 Watafiti wa lugha ya kufundishia.....	11
1.6.5 Wanafunzi na walimu.....	11
1.7 Mipaka ya Utafiti	12

1.8	Vikwazo vya Utafiti	12
1.9	Muhtasari.....	13
SURA YA PILI.....		14
2.0	MAPITIO YA KAZI TANGULIZI	14
2.1	Utangulizi	14
2.2	Mapitio ya Kazi Tangulizi Kinadharia.....	14
2.1.1	Mambo Yanayochangia Wanafunzi Kukosa Maarifa ya elimu ya Sekondari nchini Tanzania Kinadharia	16
2.1.2	Tafiti kuhusu Mambo Yanayochangia Wanafunzi kukosa Maarifa ya Elimu ya Sekondari nchini Tanzania	19
2.1.3	Athari za Kutotumia Lugha ya Kiswahili Kufundishia Elimu ya Sekondari.....	21
2.1.4	Mapitio ya Kazi Tangulizi za Tafiti Mbalimbali	22
2.1.5	Athari ya Kutotumia Lugha ya Kiswahili Kufundishia Elimu ya Sekondari.....	24
2.1.6	Changamoto Zinazowakabili Walimu na Wanafunzi Kutokana na Kutotumika kwa Kiswahili katika Ufundishaji wa Elimu ya Sekondari	28
2.1.7	Mapitio ya Kazi Tangulizi Kisera	30
2.1.8	Mambo Yanayochangia Wanafunzi Kukosa Maarifa ya Elimu ya Sekondari Nchini Tanzania	30
2.1.9	Athari ya Kutokutumia Lugha ya Kiswahili Kufundishia Elimu ya Sekondari.....	34
2.1.10	Changamoto Zinazowakabili Walimu Kutokana na Kutotumika Kwa Kiswahili Katika Ufundishaji wa Elimu ya Sekondari	35

2.2	Kiunzi cha Nadharia	37
2.3	Nadharia ya Uzamaji	37
SURA YA TATU		40
3.0	MBINU ZA UTAFITI	40
3.1	Utangulizi	40
3.2	Mkabala wa Utafiti	40
3.3	Eneo la Utafiti	40
3.4.1	Sampuli.....	42
3.4.2	Usampulishaji.....	49
3.5	Mbinu za Kukusanya Data	50
3.5.1	Mbinu ya Maktabani	52
3.5.2	Mbinu ya Hojaji	52
3.5.3	Mbinu ya Mahojiano	53
3.6	Vyanzo vya Data	55
3.6.1	Data za Msingi	55
3.6.2	Data Upili	55
3.7	Uchambuzi wa Data	56
3.8	Maadili ya Utafiti	56
3.9	Hitimisho	57
SURA YA NNE.....		58
4.0	UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA	58
4.1	Utangulizi	58
4.2	Mambo yanayochangia Wanafunzi Kukosa Maarifa ya Elimu ya Sekondari.....	59

4.2.1	Kiswahili Kutotumika Kufundishia Elimu ya Sekondari Tanzania	59
4.2.2	Kiswahili Kutopewa Umuhimu wa Kutumika Kufundishia Elimu ya Sekondari.....	62
4.2.3	Kutoeleweka Vizuri Lugha ya Kiingereza katika Shule za Sekondari	63
4.2.4	Data Zilizotokana na Mahojiano.	65
4.2.5	Majumuisho ya Lengo la Kwanza la Utafiti	66
4.3	Athari ya Kutokutumika Kwa Lugha ya Kiswahili Kufundishia Elimu ya Sekondari.....	68
4.3.1	Ufumbuzi wa athari za Kutofundishia Lugha ya Kiswahili.....	72
4.4	Changamoto Zinazowakabili Walimu na Wanafunzi Kutokana na Kiswahili Kutotumika Kufundishia Elimu ya Sekondari	75
4.4.1	Mambo Yanayozuia Lugha ya Kiswahili Kufundishia Sekondari.....	80
4.4.2	Vikwazo vya Kiswahili kuwa Lugha ya Kufundishia Sekondari.	81
4.4.3	Majibu ya Mahojiano	82
4.4.4	Majumuisho ya Lengo la Tatu la Utafiti	83
4.5	Hitimisho	84
	SURA YA TANO	86
	5.0. MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	86
5.1	Utangulizi	86
5.2	Muhtasari wa Utafiti.....	86
5.3	Hitimisho	88
5.4	Mapendekezo	90
5.4.1	Mapendekezo ya Jumla	90
5.4.2	Mapendekeo kwa Tafari Zijazo.....	91

MAREJEO	92
VIAMBATISHO	102

MAJEDWALI

Jedwali 3.1: Takwimu ya Matokeo ya Kidato cha Nne 2012 Shule A na B.....	44
Jedwali 3.2: Takwimu ya Matokeo ya Mwaka, 2013 kwa Shule A na B.....	45
Jedwali: 4.2: Majibu ya Walimu na Wanafunzi Juu ya Mambo Yanayochangia Wanafunzi Kukosa Maarifa ya Elimu ya Sekondari	60
Jedwali: 4.3: Matokeo ya Walimu na Wanafunzi Kuhusu Athari ya Kutokutumika kwa Lugha ya Kiswahili Kufundishia Elimu ya Sekondari.....	69
Jedwali: 4.4: Maoni ya Walimu na Wanafunzi juu Ufumbuzi wa athari za Kutofundishia Elimu ya Sekondari kwa Lugha ya Kiswahili	73
Jedwali 4.5: Majibu ya Walimu na Wanafunzi Kuhusu Changamoto Zinazowakabili Walimu Na Wanafunzi Kutokana Na Kiswahili Kutotumika Kufundishia Elimu ya Sekondari	76

KIELELEZO

Kielezo 3.1: Ramani ya Jiji la Mwanza Kuonyesha Mahali Ilipo Wilaya ya

Ilemela 41

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Sura hii imegawanyika katika sehemu nane ambazo ni; utangulizi, usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, mipaka ya utafiti na vikwazo vya utafiti. umuhimu wa utafiti kwa wadau mbalimbali wa elimu.

1.2 Usuli wa Tatizo

Kwa mjibu wa Galabawa na Lwaitama(2005) Kiingereza ni lugha ya kufundishia katika shule za sekondari Tanzania kama ilivyotamkwa katika sera ya elimu ya Taifa 1995 na katika pendekezo la sera ya elimu ya 2014 inayotamka kwamba, lugha ya kufundishia elimu ya sekondari iendelee kuwa Kiingereza na Kiswahili kiwe ni somo la lazima kwa kiwango hicho.

Naye Neke, (2003) alihoji kwamba, kuendelea kutumia lugha ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia katika elimu ya sekondari nchini Tanzania ni kuwafanya wanafunzi wa kiwango hiki kuwa na ugumu wa kuelewa kanuni za kisayansi na kiteknolojia kutokana na ujuzi mdogo wa lugha inayotumiwa kufundishia. Anaendelea kueleza kuwa, baadhi ya walimu wa sekondari hufundisha katika Kiswahili ili kurahisisha somo badala ya kutumia Kiingereza kilichopewa dhima ya kuwa lugha ya kufundishia ingawa mitihani hutungwa katika lugha ya Kiingereza. Hali hii inadhihirisha kwamba, kutokuelewa lugha ya kufundisha kunachangia kwa kiasi kikubwa kushindwa kufaulu mitihani kwa wanafunzi.

Brock-Utne na wenzie, (2005) wanasema kuwa, ujuzi katika lugha ya kufundishia ni jambo muhimu. Kwa sababu, inawezesha, wanafunzi kuuliza maswali, kujadili na kubainisha mada na wenzao au mwalimu, kufikiri kwa kina namna maarifa mapya yanavyo husiana na yale waliyo nayo. Kwa upande mwingine kukosa umilisi wa lugha ya kufundishia ni kipingamizi kwa wanafunzi kuelewa jinsi ya kuunda maswali, hoja za mijadala na kufikiri kwa kina.

Halikadhalika, O-Saki, (2003) anadai kwamba, pale walimu na wanafunzi wanapofanya kazi katika mazingira ya lugha wasiyokuwa na umilisi wake ni vigumu kuelewana na ni vigumu kwa mwanafunzi kuelewa dhana ya mada iliyofundishwa. O-saki (keshatajwa) anadai kwamba, kimsingi umilisi wa lugha ya kufundishia ni njia mojawapo ya kupitishia maarifa ya mfumo wa elimu ya jamii, kanuni za misamiati na utamaduni wa jamii husika.

Rubagumya (2003) anasema kwamba, walimu wengi wa shule za Sekondari Tanzania hawana uwezo wa kutumia lugha ya Kiingereza kwa ufasaha katika kufundishia, badala yake huchanganya lugha mbili ili waweze kufafanua mada darasani. Rubagumya (keshatajwa) anafafanua kuwa, wanafunzi wanawaelewa vizuri walimu wao pale ambapo mafunzo hutolewa kwa lugha ya Kiswahili. Anaendelea kusema kuwa, tatizo huanzia pale wanafunzi wanapoanza elimu ya sekondari bila ya kuwaandaa vya kutosha kukabiliana na matumizi ya lugha ya kigeni, matokeo yake, wanafunzi wengi huanza kupoteza mwelekeo tangu kidato cha kwanza kwa kutoelewa vizuri masomo kutokana na ushiriki wao mdogo pale wanapofundishwa kwa lugha ya kigeni.

Lugha ya Kiswahili imekuwa, na ina uwezo mkubwa wa kuweza kupewa dhima ya kufundishia-sekondari. Rubanza (1979), Mochiwa (1979), Mekacha (1995) na (1997) wanaonyesha kwamba, watoto wengi wa vijijini wenye uelewa wa Kiswahili kama lugha ya pili umeongezeka. Idadi ya watanzania wanaotumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya kwanza inaongezeka kwa haraka pia. Aidha, Brock-Utne (2000) na Brock-Utne (2002) anadai kwamba, wanafunzi wanaelewa vizuri wanapofundishwa katika lugha ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Brock-Utne (2003) lugha zinazotumika kufundishia katika madarasa ya Afrika ni lugha ambazo hazitumiwi na wanafunzi wawapo nje ya shule na wala hawaelewi kwa usahihi. Zaidi ya hayo walimu wenyewe hawaitumii lugha hiyo nje ya mazingira ya darasa. Kwa mujibu wa Qorro (2005) Kiswahili ni lugha inayopaswa kutumiwa katika nyanja zote za mawasiliano ya kitaifa hasa katika shule. Ni lugha inayofahamika vizuri kwa wanafunzi na walimu. Qorro (2005) anaendelea kuisisitiza kwamba, nchi nyingi duniani ambazo hutumia lugha zake huonyesha mafanikio katika uchumi, siasa na jamii. Kwa mfano, China ni mojawapo ya nchi inayoonyesha mfano mzuri wa kutumia lugha yake kufundishia watu wake na matokeo yake ni kuwa na maendeleo makubwa ya kiuchumi.

Aidha, Qorro (keshatajwa) anabainisha kwamba, Tanzania kuendelea kutumika lugha ya kigeni (Kiingereza) kufundishia elimu ya Sekondari ni dalili ya kushindwa kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari, na kusababisha wale wanao tumia lugha hiyo kushindwa kujifungamanisha na wanajamii yao. Qorro (keshatajwa) anaendelea kudai kwamba, wanafunzi wanapofundishwa kwa lugha

wasiyoijua, wanakosa maarifa ya kuendeleza mambo yao ya msingi ya mila na desturi zao, kushindwa kujiamini na kukosa uhuru wa kifikra na kimaarifa, na mbaya zaidi kuathiriwa na tamaduni za kigeni zinazoambatana na matokeo ya matumizi ya lugha hizo za kigeni.

Kwa mujibu wa Qorro (keshatajwa) kama alivyomnukuu Rubagumya (2003) Kiswahili ni lugha inayopaswa kutumiwa katika nyanja zote za mawasiliano ya kitaifa hasa katika shule. Kutotumika kwa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika ngazi zote za elimu kuna madhara makubwa. Walimu hushindwa kujieleza vizuri kwa sababu ya kutumia lugha ya Kiingereza ambayo wengi wao hawana umilisi wake wa kutosha na hivyo kusababisha mawasiliano duni baina yao na wanafunzi ambao pia wengi wao hawamudu Kiingereza vizuri.

Pia, tafiti zilizokwisha kufanywa na wanazuoni wengi wakiwemo; Qorro (2005), Malekela (2003 & 2004), na Mwinsheikhe (2003) wanajadili kuwa, matumizi ya lugha ya kigeni katika kufundishia yana madhara makubwa kwa ujenzi wa jamii imara, kwa maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na ukuzi wa sayansi na teknolojia kwa sababu wanafunzi hukosa kupata stadi kamili za somo husika.

Vilevile Mwinsheikhe (keshatajwa) anadai kwamba, walimu wengi kutotumia lugha ya Kiswahili kufundishia masomo yote huchangia kutokueleweka vema kile wanachofundisha darasani, hawana umilisi wa kutosha wa lugha ya Kiingereza, hufikiri na kuunda dhana zote kwa Kiswahili kisha kuzitafsiri kimawazo katika akili zao katika Kiingereza ambacho dhana zake kuhusu mambo wanayojifunza hayako

akilini mwao tangu awali. Matokeo yake dhana zinazoundwa akilini siyo sahihi kutokana na mawasiliano kiakili kukwazwa na lugha wasiyo na ujuzi. Nchini Tanzania, masomo na mafunzo hufunzwa kwa Kiingereza na Kiswahili kinyume cha matakwa ya sera. Wanafunzi wengi wanapojifunza wao wenyewe nje ya madarasa hutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kidogo. Hii inaonyesha kuwa, Kiswahili ndiyo lugha inayoeleweka kwa wanafunzi na walimu.

Vilevile, Mekacha, (2000) anasema kwamba, watoto wengi, hata wa vijijini wanakuwa wanafahamu vizuri lugha ya Kiswahili wanapoanza masomo ya shule ya msingi.–Msanjila na wenzie (2009) wanadai kwamba, hadi wakati huu, lugha ya Kiswahili imekwisha ingizwa katika mifumo miwili ya kompyuta ijulikanayo kama *Linux* na *Microsoft*.

Msanjila na wenzie (keshatajwa) anadai kwamba, Kuingizwa kwa Kiswahili katika mifumo hii maana yake ni kwamba mtumiaji anaweza kuvinjari mifumo hiyo ya kompyuta kwa Kiswahili akiamua kufanya hivyo, na kubwa zaidi ni kielelezo cha ukuaji wa lugha hiyo. Wanaendelea kusema kwamba, uwezo wa Kiswahili kuingia katika teknolojia ya habari na mawasiliano, kunawathibitishia wenye mamlaka na jamii kwa ujumla kwamba Kiswahili kina uwezo wa kukabili hata mambo yasiyokuwa ya asili yake. Aidha, lugha ya Kiswahili ina nguvu ya kuwapa watumiaji wake uwezo wa kutumia teknolojia hiyo kufanyia mambo yao na si yale yenye asili ya kigeni tu. Msanjila na wenzie (wameshatajwa), wanahitimisha kwa kusema kwamba, mafanikio haya kwa jamii yanakiweka Kiswahili katika nafasi nzuri ya kupewa nafasi ya kutumika katika elimu ya sekondari kama zilivyopewa hizo lugha

kubwa zilizopiga hatua kisayansi na kiteknolojia. Nafasi kama hiyo itaipa lugha hii fursa mpya ya kuweza kutumiwa pia kujenga maendeleo ya jamii kwenye misingi ya kiutamaduni ya jamii ya nchi ya Tanzania. Senkoro (2004rb) anatoa hoja kwamba, pamoja na serikali kuchochea kwake uanzishwaji wa vyombo rasmi vya kuendeleza lugha ya Kiswahili, haikuandamana na sheria ya kukazia utekelezaji wa matakwa na mahitaji ya lugha ya hadhi hiyo, ambayo ni pamoja na kufundishia elimu za viwango vyote. Jambo lingine ni kuchelewa kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari.

Ripoti ya tume ya Makweta ya 1982, ilipendekeza kwamba Kiswahili kianze kutumika kama lugha ya kufundishia elimu ya sekondari kuanzia mwaka 1985. Kabla ya mpango huo kutekelezwa serikali ilitoa mwongozo kwamba Kiingereza kiendeleo kutumika katika sekondari na vyuo. Tamko hilo limezua mjadala ambao unaendelea hadi leo. Inaonekana kwamba, Tangu Tanganyika ipate Uhuru, jitihada nyingi zimeshafanyika za kukifanya Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia elimu ya sekondari lakini bado hakuajwa na mafanikio ya kiutekelezaji mpaka sasa.

Qorro (2003) lugha ya kwanza huwa ni chombo cha kumwezesha mhusika kung'amua na kueleza mtazamo na hisia zake za ndani kwa kila kinachomfikia au kinachotolewa kwake. Uwezo huu wa kung'amua na kueleza mtazamo na hisia za ndani kuhusu maarifa, ndiyo msingi wa ubunifu na ugunduzi. Kwa upande wa Tanzania, lugha ya Kiswahili ni ya kwanza kwa baadhi na ni ya pili kwa baadhi ya watanzania. Lakini, lugha inayotumika kufundishia elimu ya sekondari ni ya tatu kwa wananchi walio wengi. Hali hiyo husababisha walimu kukosa uwezo unaostahili

wa kufundisha masomo ya sekondari. Kwa hiyo, Wanafunzi kulazimika kukariri kwa ajili ya kufaulu mitihani bila kuelewa vema. Hali hii inaviza ufahamu wao na jamii kukosa maarifa ya kiwango cha elimu ya Sekondari nchini.

Hali kadhalika, Msanjila na wenzake (2009) anadai kwamba, Kiswahili ni lugha ya Taifa na ni lugha rasmi ya shughuli za serikali nchini Tanzania. Lugha hii inatumika pia Burundi, Kongo, Rwanda na Uganda, pia ni lugha ya taifa nchini Kenya. Aidha, lugha hii inakubalika na kupendwa kote ulimwenguni kiasi kwamba hata vyombo vya habari vya kimataifa hutumia lugha ya Kiswahili kutolea matangazo mfano mzuri ni BBC na sauti ya Amerika.

Kwa mujibu wa Mwinsheikhe, (2003) kutotumia lugha inayofahamika vema kwa wanafunzi kufundishia, kunafanya wanafunzi wakose maarifa ya kuendeleza mambo yao ya msingi wa mila na desturi zao, kushindwa kujiamini na kukosa uhuru wa kifikra na kimaarifa, na mbaya zaidi kuathiriwa na tamaduni za kigeni zinazoambatana na matokeo ya matumizi ya lugha za kigeni. Vilevile, walimu wengi hawana uwezo wa kufundisha masomo kwa lugha ya kigeni.

Aidha, tafiti za (Roy-Campbell na Qorro, 1987, Mwinsheikhe 2002, Vuzo, 2002, Galabawa na Lwaitama, (2005) ulibaini kwamba, wanafunzi wa shule za Sekondari nchini Tanzania wanafaulu mitihani zaidi pale wanapofundishwa kwa Kiswahili kuliko kufundishwa kwa lugha ya Kiingereza. Kwa hali hii ni dhahili kwamba, upo uhusiano kati upatikanaji wa maarifa yanayokusudiwa na lugha ya kufundishia.

1.3 Tatizo la Utafiti

Kutotumika kwa lugha ya Kiswahili katika mchakato wa kufundishia elimu ya Sekondari nchini Tanzania ni tatizo kubwa. Wanafunzi wanakosa maarifa, stadi na ujuzi unaostahili kutokana na kikwazo cha mawasiliano yasiyo fanisi baina yao na walimu wao darasani. Walimu na wanafunzi wa Sekondari hufanya mawasiliano nje ya darasa kwa lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wa Sekondari walio wengi nchini hawana uwezo wa kujieleza kwa lugha ya Kiingereza kinachotumiwa kufundishia. Aidha, walimu wengi hawana ujuzi wa kufundishia Kiingereza. Hili ni tatizo kubwa, kwa kuwa lugha ndiyo chombo kikuu cha mawasiliano baina ya walimu na wanafunzi. Kwa mujibu wa Rubagumya, (2003) wanafunzi wa Tanzania wanaelewa walimu wao vizuri pale mafunzo yanapotolewa kwa lugha ya Kiswahili. Tafiti zilizokwisha fanywa na Kamugisha na Mateng'e (2014) zilijikita zaidi kutafuta ulinganifu wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza, lugha ya kufundishia katika gazi zote za elimu, na lugha ya kufundishia masomo ya sayansi.

Hata hivyo tafiti hizo hazikufanyika katika shule za jiji la Mwanza Wilaya ya Ilemela. Kwa jumla hakuna utafiti uliokwisha fanyika wa moja kwa moja wa kuchunguza uhusiano baina ya kutotumika kwa lugha ya Kiswahili katika ufundishaji wa masomo katika shule za sekondari na kushindwa kwa wanafunzi kupata maarifa yaliyokusudiwa. Lugha ya kufundishia elimu ya sekondari nchini Tanzania imekuwa na lawama nyingi hasa kutokana na matokeo mabaya ya mitihani ya Taifa. Kamugisha na Mateng'e (keshatajwa) wanadai kwamba, matokeo mabaya ya mtihani wa kidato cha nne ya mwaka 2014 yalichangiwa na lugha ya kufundishia.

Kutokana na hali hiyo, mapendekezo yakatolewa ya kubadilisha lugha ya kufundishia iwe ni Kiswahili.

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una malengo mawili, yaani; lengo kuu na malengo mahususi. Sehemu ifuatayo inajadili malengo hayo;

1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza uhusiano baina ya kutotumika kwa Kiswahili katika ufundishaji wa masomo katika shule za sekondari na kushindwa kwa wanafunzi kupata maarifa yaliyokusudiwa.

1.4.2 Malengo mahususi ya utafiti

- i) Kubainisha mambo yanayo changia wanafunzi kukosa maarifa ya elimu ya sekondari,
- ii) Kubainisha athari zitokanazo na kutokutumika kwa lugha ya Kiswahili katika kufundishia elimu ya sekondari na
- iii) Kujadili changamoto zinazowakabili walimu na wanafunzi zitokanazo na kutotumika kwa Kiswahili katika ufundishaji wa elimu ya sekondari.

1.5 Maswali ya Utafiti

Maswali ya utafiti yatachunguza yafuatayo:

- i) Ni kwa nini hadi leo kiswahili hakitumiki kufundishia elimu ya sekondari Tanzania?

- ii) Je, nini athari zitokanazo na kutotumia lugha ya kiswahili kufundishia elimu ya sekondari nchini?
- iii) Ni changamoto gani zinazowakabili walimu na wanafunzi kwa kutotumika kwa Kiswahili katika ufundishaji wa elimu ya sekondari?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu umekuja kwa wakati mwafaka, ambapo kuna mijadala mikali juu ya lugha ya kufundishia elimu ya sekondari. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kuwa na umuhimu kwa kwa wadau wa elimu kama ifuatavyo:-

- i) Walimu watamaliza mada za mihtasari ya masomo kwa wakati kwa kuwa watumia lugha inayoeleweka kwao na wanafunzi
- ii) Wazazi wataweza kufuatilia maendeleo ya watoto wao kitaaluma
- iii) Ufaulu wa wanafunzi utaongezeka na uwezo wa kuchangia mawazo darasani utaongezeka kwakuwa lugha itakayotumika itaeleweka vizuri kwao

1.6.1 Wanataaluma

Utafiti huu utachochea wanataaluma wa kitanzania kutafsiri vitabu mbalimbali ili kupata machapisho mengi katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu utaweza kuhamasisha wataalamu wa Kiswahili vyaoni kuunda idara za kutafiti na kuandaa walimu wenye ujuzi wa kufundisha lugha ya Kiswahili na kuandaa vitabu katika lugha ya Kiswahili.

1.6.2 Watunga Sera ya elimu

Utafiti huu utawawezesha watunga sera kuchukua hatua za makusudi kurekebisha sera ya elimu kuhusu lugha ya kufundishia katika shule za Sekondari. Utafiti huu pia

utasaidia wizara ya elimu kufanya maamuzi ya lugha stahili ya kufundishia elimu ya sekondari ili kupunguza ama kuondoa kabisa athari zitokanazo na matumizi ya lugha ya kigeni kufundishia elimu ya sekondari nchini. Athari hizo ni pamoja na wanafunzi kushindwa kuelewa wanachofundishwa, kushindwa kuwasiliana na walimu darasani na nje ya darasa, na walimu kukosa umilisi wa lugha.

1.6.3 Jamii ya Watanzania

Utafiti huu utatoa mchango mkubwa kwa jamii ya watanzania katika kutafuta mustakabali wa hali ya elimu nchini kwa kupata maendeleo yatokanayo na ustadi wa wanafunzi walioelimishwa kwa lugha yao. Kwa kuwa lugha itakayotumika kufufundishia elimu ya sekondari itakuwa ni ile inayofahamika vizuri na wanajamii wataweza kufuatilia maendeleo ya elimu ya watoto wao.

1.6.4 Watafiti wa lugha ya kufundishia

Utafiti huu utawachochea watafiti wengine watakao penda kufanya utafiti katika uwanja wa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari, ili kuziba mapengo yaliyoachwa na utafiti huu.

1.6.5 Wanafunzi na walimu

Utafiti huu utasaidia kuchochea ufaulu na mahudhurio ya wanafunzi kwa kuwa watagundua ni vikwazo gani vinavyosababisha kushindwa kufaulu na vile vinayowakatisha tamaa ya kuhudhuria shule. Utafiti huu pia utasaidia walimu kugundua athari na vikwazo vinavyo wafanya wanafunzi kukosa mawasiliano kamili na hatimaye wanafunzi kutopata maarifa kamili. Kwa kufanya hivyo kutaweka

mazingira kuwa rafiki kwa walimu na wanafunzi pale itakapo amriwa kuwa lugha ya kufundishia ni Kiswahili kinachoeleweka kwa wote. Aidha, wanafunzi wa shule za sekondari nchini Tanzania watajengewa mazingira mazuri ya kukuza stadi na maarifa yao kwa kiwaango cha elimu ya sekondari.

1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unahusu lugha ya kufundishia elimu ya Sekondari. Ingawa ufundishaji na ujifunzaji hufanyika kwa wakati mmoja. Utafiti huu umeangalia suala la ufundishaji tu kwani hili ni jukumu la mwalimu zaidi wakati ujifunzaji unamhusu mwanafunzi tu. Aidha, mwalimu ndiye anayetumia lugha ya kufundishia ambayo inabeba maana na maarifa, ujuzi na stadi ambazo mwanafunzi anatakiwa kuzipata kupitia lugha ya kufundishia na inayoeleweka vema kwa mwalimu na mwanafunzi pia.

1.8 Vikwazo vya Utafiti

Katika kufanya utafiti huu, mtafiti alikutana na vikwazo vya muda mfupi wa kufanya utafiti na uhaba wa fedha ambavyo vililikuwa nje ya uwezo wake. Kwa kuwa utafiti ulifanyika wakati mtafiti akiwa kazini, wakati mwingine alibanwa na majumu ya mwajiri. Pia wakati mwingine mtafiti alihitaji kusafiri kwenda wilayani ili kupata data za ziada ili kukamilisha utafiti huu hivyo gharama kuwa kubwa ya kwenda mara kwa mara. Aidha, baadhi ya walimu hawakuwa wazi juu ya uwezo wao katika kutumia lugha ya kufundishia elimu ya Sekondari. Kwahiyo, mtafiti alilazimika kufanya mahojiano kwa lugha mbili za Kiswahili kwa baadhi ya hoja na Kiingereza kwa hoja nyingine. Mbinu hii ilisaidia kupunguza kikwazo cha walimu kutoa kuwa wazi, kwa kiasi kikubwa japokuwa bado ilikuwa ni kikwazo katika utafiti huu. Pia

mtafiti alitatusa matatizo ya mwajili kwa kuomba likizo ili kukamilisha kazi ya utafiti. Mtafiti pia alitumia bajeti iliyo pangwa mapema kukamilisha kazi hii, hivyo vikwazo vyote vikatatuliwa.

1.9 Muhtasari

Tukihimisha sura hii ya kwanza tunaweza kusema kwamba. Katika sura hii tumemejadili vipengele mbalimbali ambayo ni usuli wa tatizo wa tatizo umejadiliwa kwa kina kuhusu lugha ya kufundishia kuwa ni chombo cha kubebea maarifa na stadi za mwanafunzi. Kwamba kuna matatizo makubwa kwa wanafunzi na walimu pale lugha ya kufundishia inapokuwa haieleweki vema. Tatizo la utafiti limejadiliwa kwamba, kutotumia lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari ni tatizo kubwa. Malengo ya utafiti huu. Maswali ya utafiti. Umuhimu wa utafiti pia umejadiliwa. Kiunzi cha nadharia ambacho ni uzamaji. Mwisho tumejadili kwa kina kuhusu mipaka na vikwazo vya utafiti huu.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

2.1 Utangulizi

Sura hii imejikita katika mapitio ya kazi mbalimbali zilizopita za kinadharia, kisera na za kitafiti zilizowahi kufanyika kuhusu lugha ya kufundishia katika shule za Sekondari ndani na nje Tanzania. Kwa hiyo sura hii imegawanyika katika mbili; mapitio kuhusu lugha ya kufundishia na kiunzi cha nadharia. Sehemu ya kwanza imegawanyika katika sehemu zifuatazo: Kwanza, dhana ya lugha ya kufundishia kwa jumla imejadiliwa. Pili Mambo yanayochangia wanafunzi kukosa maarifa ya sekondari. Tatu, athari za kutotumia lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari pia zimejadiliwa. Nne, changamoto zinazowakabili walimu na wanafunzi kutokana na kutotumika kwa Kiswahili katika ufundishaji wa elimu ya sekondari nao umejadiliwa kwa mapana. Aidha, mapitio ya kazi tangulizi kisera pia imejadiliwa katika sura hii. Mijadala yote ilianguzia hali ya ndani na nje ya Tanzania ili kupata upana wa mawazo kuhusu mada ya utafiti huu.

2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi Kinadharia

Lugha ya kufundishia ni lugha inayotumiwa na mwalimu kufundishia wanafunzi. Zhou na Sun, (2004). Aidha, lugha ya kufundishia ni lugha iliyoteuliwa kutolea elimu kwa taifa zima au sehemu ya taifa na kwa kiwango maalum cha elimu au kwa viwango vyote vya elimu. Hoja hizo zinaungwa mkono na Msanjila na wenzie (2009) wakidai, kwamba, lugha ya kufundishia ni lugha inayotumiwa kutolea maarifa katika mfumo wa elimu. Lugha hiyo, ndiyo inayotumika kujenga mfumo wa

mwasiliano katika elimu na kuwasilisha stadi na maarifa ya msingi kwa umma, kubuni na kuendeleza maarifa.

Msanjila na wenzie (wameshatajwa) kadhalika wanaendelea kudai kwamba, lugha ya kufundishia huwa ni chombo cha kuwapa watu uwezo na nguvu kiutamaduni na kisayansi. Aidha, Msanjila na wenzake (wameshatajwa) wanaendelea kudai kwamba, lugha ya kufundishia ina dhima kubwa katika maendeleo ya jamii kwa kukuza fikra pevu zilizo msingi wa ubunifu na ugunduzi.

Msanjila na wenzie (2009) wanasema kwamba, lugha ya kufundishia ni lugha inayotumika kufundishia masomo katika mfumo wa elimu wa nchi. Matumizi ya lugha kama lugha ya kufundishia katika mfumo wa elimu, zaidi ya kuwasaidia wanaojifunza kuendeleza vipaji vyao vya ubunifu, huwa pia ndiyo njia ya kuendeleza lugha hiyo ili kukabili taaluma za sayansi na teknolojia. Naye Qorro (2006) anatoa hoja kwamba, lugha ya kufundishia ni chombo cha kupitishia elimu kutoka kwa walimu kwenda kwa wanafunzi na miongoni mwa wanafunzi wenyewe. Hali kadhalika, Qorro (2005) anadai kwamba, pale wanafunzi wanaposhindwa kuongea lugha ya kufundishia hakika hawataweza kujifunza. Mtaalamu huyo (keshatajwa) aliendelea kudai kwamba, lugha yenye ufanisi na ya kuleta matokeo yanayotakiwa ni ile tu inayofahamika vizuri kwa walimu na wanafunzi. Anaendelea kudai kwamba, lugha ya kufundishia masomo yote sekondari iwe ni kswahili kinachoeleweka wa wanafunzi wengi na walimu pia. Naye, Senkoro (2004) anatoa hoja kwamba, lugha inayoweza ujifunzaji na ufundishaji inatakiwa iwe lugha inayoeleweka vizuri kwa walimu na wanafunzi. Vilevile, utafiti wa Senkoro

(keshatajwa) uliofanyiwa katika mikoa ya Iringa, Manyara, Zanzibar na Kagera aligundua kuwa wanafunzi wanashindwa kuelewa kile kinachofundishwa na walimu kwa lugha ya Kiingereza. Aidha, utafiti wa Galabawa na Lwaitama wakinukuliwa katika Brock–Utne na wenzake (2005) waligundu kwamba, wanafunzi wanaelewa masomo ya sayansi na kufaulu zaidi pale tu wanapofundishwa kwa lugha ya Kiswahili. Mapendekezo yake yaliwataka watafiti wabaada yake wajihusishe katika utafiti wa lugha ya Kiswahili kuwa ya kufundishia elimu ya Sekondari. Pendekezo hili lilitoa mwanya kwangu kufanya utafiti ili kugundua kama kuna uhusiano wa lugha ya kufundishia na maarifa yanayokusudiwa kupatikana kwa kiwango cha Sekondari nchini.

2.1.1 Mambo Yanayochangia Wanafunzi Kukosa Maarifa ya elimu ya Sekondari nchini Tanzania Kinadharia

Mambo yanayochangia wanafunzi kukosa maarifa ya sekondari ni kufundishwa kwa kutumia lugha wasiyo na umilisi wake. Kwa mujibu wa Mekacha, (2000) lugha ni nyenzo inayoweza binadamu kufikiri, kuwasiliana, kuhifadhi na kurithisha maarifa. Lugha ni nyenzo muhimu sana katika kufikiri. Kila mara binadamu anapotumia lugha hufikiri kwanza, anapotaka kusema lolote hufikiria kwanza jambo la kusema namna ya kusema ili ujumbe aliokusudia kuuwasilisha ufikishwe kwa msikilizaji bila utata.

Kwa hiyo basi, haiwezekani watu kufikiri bila kutumia lugha. Mtu anapofundishwa katika lugha anayoifahamu vizuri huelewa anachofundishwa na huweza kueleza vyema alichojifunza kwa maneno yake na hata huweza kuwa na ugunduzi kwa vile

hufikiria kwa kutumia lugha anayoielewa. Vilevile, Msanjila na wenzake (2011) lugha ya kufundishia inapoteuliwa visivyo, huwa kunajitokeza vikwazo vingi ambavyo huathiri ufanisi katika kutoa, kubuni na kuendeleza maarifa. Vikwazo hivyo ni wajifunzaji kuwa na mtazamo wa kutoipenda lugha hiyo, kuondoa juhudi ya kuijua na kuitumia, hivyo kukwamisha michakato ya ujenzi na utoaji wa maarifa muhimu kwa maendeleo ya jamii.

Hivyo basi, ili mwanafunzi apate maarifa na uwezo wa kujitambua na kung'amua kile kilichofundishwa na mwalimu wake lazima awe na umilisi wa lugha ya kufundishia. Maelezo hayo yanaungwa mkono na Mekacha (2000) kwa madai kuwa, watu hufikiri katika lugha na lugha hutumika katika kufikiri, lugha ndiyo nyenzo ya kuwasilisha na kuweka wazi fikra na mawazo. Kutokana na hali hii ni wazi kuwa lugha na kufikiri ni mambo yanayofungamana. Aidha, Mekacha (amesha tajwa):

*“Lugha na kufikiri ni mambo yaliyofungamana mno kiasi kwamba haiwezekani
Kujadili mojawapo bila kulihusisha na jingine, kusema kuna hudumia fikra na Fikra hujibainisha katika kusema (UK 3)”*

Maelezo hayo yanatoa picha kwamba, lugha ya kufundishia inatakiwa iwe ndiyo inayowezesha mwanafunzi kufikiri na kuamua kipi akiseme kwa wakati ulio sahihi. Prah (2003) anaeleza kwamba, lugha ya kwanza ikitumika kama lugha ya kufundishia huwezesha watu kujiaamini. Kwa hali hiyo, lugha ya kufundishia ina dhima kubwa katika maendeleo ya jamii kwa kukuza fikra pevu zilizo msingi wa ubunifu na ugunduzi.

Prah (amesha tajwa) anaendelea kudai kwamba, lugha ya kufundishia ndiyo inayotumika kujenga mfumo wa elimu na ndiyo lugha inayotumiwa kuwasilisha

stadi na maarifa ya msingi ya umma na ndiyo ya kuimarisha ubunifu na kuendeleza maarifa ya wajifunzaji. Kwa hali hii basi, huwa ndiyo lugha ya kulimbikiza na kuhifadhi maarifa. Naye Tikolo (2012) anatoa hoja kwamba, ufahamu wa wanafunzi wa lugha aliyoizoea wakati wa kukua kwake inaweza kuwa ndiyo msingi wa ujifunzaji mzuri wa baadaye, pale anapounganisha na ujuzi wa mwalimu wake.

Naye Rubanza (2002) anadai kwamba, wanafunzi wa Tanzania hupoteza ujuzi wa Kiingereza mara tu wanapohitimu elimu yao, kwasababu jamii inayowazunguka haitumii lugha Kiingereza, hivyo kupoteza lugha hiyo baadaya muda mfupi wa kumaliza elimu ya sekondari.

Kwa mujibu wa Vuzo (2002) lugha ya kufundishia inaweza kuathiri uwezo wa ujifunzaji kufafanua maelekezo na maswali. Aidha, mwalimu na mwanafunzi wanaathiriana pale Kiswahili kinapo kuwa lugha ya kufundishia na wanafunzi wengi wanakuwa wepesi kuelewa na kujibu maswali yanayoulizwa katika lugha ya Kiswahili. Msanjila na wenzake (2011) wanadai kuwa, lugha ya kufundishia inapowekewa mipaka ya matumizi yake huwa kuna kosekana mwendelezo katika utoaji, ubunaji na uendelezaji wa maarifa.

Maelezo ya wanaisimu hao hapo juu yanadhihrisha kwamba lugha inayotumiwa kufundishia ndiyo inamfanya mwanafunzi na mwalimu waathiriane na hivyo mwanafunzi kupata maarifa kamili ikiwa lugha inayotumiwa na mwalimu kufundishia inaeleweka vema kwa mwalimu na mwanafunzi.

2.1.2 Tafiti kuhusu Mambo Yanayochangia Wanafunzi kukosa Maarifa ya Elimu ya Sekondari nchini Tanzania

Tafiti tangulizi zinaonyesha kuwa lugha kufundishia elimu ya Sekondari nchini Tanzania ina udhaifu mkubwa. Zifuatazo ni baadhi ya tafiti hizo; Brock-Utline (2005) katika utafiti wake juu ya lugha mbili za kufundishia katika madarasa ya shule za sekondari Tanzania, aligundua kuwa lugha ya Kiingereza ilikuwa ni lugha ya pili na Kiswahili lugha ya kwanza. Kwa jumla lugha ya Kiswahili ni ya kwanza kwa baadhi na ya pili kwa wataanzania wengine. Aidha, (Brock-Utline (keshatajwa) alidai, kuwa ,mwalimu aliyekuwa anafundisha mada moja katika somo la baolojia kwa madarasa mawili ya kidato cha kwanza ambayo yalikuwa yamegawanywa katika mikondo miwili, kuliwa na shida ya kuelewa somo lililofundishwa kwa Kiingereza kuliko wale walifundishwa kwa Kiswahili. Mwalimu huyo alifundisha mkondo mmoja kwa lugha ya Kiingereza na lingine kwa kiswahili. Mwalimu alipowataka wale waliofundishwa wa Kiingereza kwenda kwenye makundi yao matano ya kawaida, kundi moja halikujua kama wao ni kundi namba tatu au namba tano. Waliuliza katika Kiswahili

“ Hatujui sisi ni kikundi cha tatu au kikundi cha tano”

Uchunguzi aliofanya katika darasa lililofundishwa katika Kiswahili ulionyesha kwamba, wanafunzi walielewa zaidi yale maarifa waliyofushwa kwa lugha ya Kiswahili na wakashiri vizuri katika kutoa michango ya mawazo yao mengi na yaliyokuwa mazuri kinyume cha darasa lilifundishwa kwa Kiingereza.

Kwa upande wa Peterson (2006) wanafunzi wana mawazo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili, kwamba wanaelewa zaidi wanapofundishwa katika lugha ya Kiswahili.

Lugha ya Kiswahili wanaitumia nje ya darasa na popote kama sehemu ya maisha yao ya kila siku, wanapofundishwa kwa lugha hiyo wanapata maarifa kamili kuliko wanapofundishwa kwa Kiingereza. Kwamba kufundishia lugha isiyofahamika kwa wanafunzi kunachangia kuharibu ubora wa elimu kwa kuwa wanafunzi hawaelewi kile kinachofundishwa. Utafiti mwingine uliofanywa na Mwinsheikhe (2003) akitaka kujua kama kutumia Kiswahili katika mchakato wa kufundisha na kujifunza kunaweza kuimalisha ushiriki na ufaulu wa wanafunzi kwa masomo ya sayansi. Aligundua kwamba, kuna tatizo la lugha katika kufundisha sayansi. Walimu wengi walikiri kutumia lugha ya Kiswahili wanapofundisha masomo hayo kinyume na sera ya elimu ya Sekondari. Aidha, wanafunzi walisema kwamba, wao wanatumia Kiswahili zaidi katika midala ya masomo yote ya sayansi. Mwinsheikhe (ameshatajwa) anahoji kwamba huo woga wa kuamua kutumia Kiswahili unatoka wapi, wakati Tanzania ilishapata kamusi ya mwongozo kwa masomo ya Biologia, Kemia na Fizikia tangu 1990 ambayo inaondoa woga kwa pale palipo kuwa na ugumu.

Hivyo basi, kuna uhusiano mkubwa baina ya lugha ya kufundishia na maarifa yanayo kusudiwa kupatikana, lugha ya kufundishia inatakiwa iwe inayofahamika vizuri kwa wanafunzi na walimu pia. Aidha, madai hayo yana toa picha juu ya elimu ya Tanzania ambayo mwanafunzi awapo shule ya msingi hufundishwa kwa lugha ya Kiswahili na anapohamia sekondari anafundishwa kwa lugha ya Kiingereza. Hali hii inamzuia mwanafunzi kuwa na mwendelezo wa maarifa aliyoyapata kutoka elimu ya msingi. Pengo linalojitokeza kutokana na mitazamo ya wataalamu hapo juu ni kwamba hawaelezi ni kwa namna gani mapitio mengi ya kazi tangulizi utaona kuwa

kazi nyingi zilizokwishafanywa zimejikita katika kutoa maelezo ya jumla kuhusu lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia elimu kwa jumla yake. Mbali na Rubagumya (1990) kudai kwamba, Kiswahili kinatakiwa kiwe chaguo la elimu ya sekondari lakini kimezuiliwa na uhaba wa vitabu na uhaba wa walimu wa kukifundisha. Hata sasa bado Kiswahili hakijapata dhima ya kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari. Pia tafiti nyingi bado nazo zimeonesha udhaifu wa kutumia lugha za kigeni kufundishia elimu, na hivyo kupendekeza lugha ya kufundishia iwe Kiswahili, si Kwa elimu ya sekondari tu, bali iwe kwa ngazi zote za elimu nchini Tanzania.

2.1.3 Athari za Kutotumia Lugha ya Kiswahili Kufundishia Elimu ya Sekondari.

Athari hizi ni zile zinazo mgusa mwalimu na mwanafunzi wa shule ya sekondari nchini Tanzania. Kwa mujibu wa Mammino (2000), ufundishaji wa elimu kwa kutumia lugha ya kigeni huathiri wepesi wa uwezo wa mwanafunzi kupata maarifa kwa upana na kwa kina. Nao Msanjila na wenzie (2011), wanadai kwamba, maarifa ni kitu kinachopanuka na kupata kina na upeo kwa njia ya matumizi ya lugha inayoeleka kwa walimu na wanafunzi. Maelezo haya ya wanaisimu hao yanaonyesha kuwa wanafunzi wa sekondari za Tanzania wanaathirika kwakukosa maarifa ya kiwango hicho kwa kuwa lugha wanayofundishiwa ni ngeni kwao. Maelezo hayo yanaungwa mkono na mwanaisimu Mekacha (2000) kwa madai kwamba, lugha ya kufundishia inapokuwa haieleweki vizuri kwa walimu na wanafunzi huathiri ufanisi katika kutoa, kubuni, na kuendeleza maarifa.

Halikadhalika, Msanjila na wenzie (keshatajwa) wanadai kwamba, pale lugha ya kufundishia inapokuwa tofauti na lugha inayofahamika katika jamii nzima, walimu wanaoitumia lugha kufundishia hushindwa kujifungamanisha na wanajamii wenzao. Wanaisimu hao wanaendelea kudai kwamba, wanafunzi pia hushindwa kutumia lugha hiyo Kung' amua, kujieleza na kukuza fikra pevu zilizo msingi wa ubunifu na ugunduzi.

Machapisho ya wataalamu mbalimbali yamesomwa na kunukuliwa hasa yale yanayoendana na mada husika. Maelezo hayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuelewa ni kwa jinsi gani lugha ya kufundishia inatakiwa iwe inafahamika vizuri kwa walimu na wanafunzi kuepuka athari za kukosekana kwa maarifa. Ingawa wataalamu hao wanatofautiana katika kueleza athari za lugha, tofauti zao hizo ni ndogo sana kuliko mchango walitoa kwa utafiti huu ili kufanya utafiti zaidi kujua uhusiano wa lugha ya kufundishia na upatikanaji wa maarifa.

2.1.4 Mapitio ya Kazi Tangulizi za Tafiti Mbalimbali

Mambo yanayochangia wanafunzi kukosa maarifa ya Elimu ya Sekondari Nchini Tanzania. Mambo yanayochangia wanafunzi kukosa maarifa ya elimu ya Sekondari nchini Tanzania ni pamoja na lugha itumika kufundishia katika shule za sekondari nchini Tanzania kwa kuwa walimu na wanafunzi hana ujuzi wa lugha hiyo. Maelezo haya yanaungwa mkono na tafiti mbalimbali za wanaisimu wafuatao:

Macdonald (1990) alibaini kwamba, ujuzi mdogo wa walimu katika lugha ya kufundishia katika nchi ya Botswana unawakosesha wanafunzi kupata maarifa ya

kujua kusoma na kuandika katika lugha ambayo haikuzoeleka kwa wanafunzi na wao wenyewe wana ujuzi mdogo wa kuitumia kufundishia.

Utafiti uliofanyiwa nchini Botswana, Prophet na Dow (1994) waligundua wanafunzi wa kidato cha kwanza waliofundishwa kwa lugha ya Kitswana walikuwa na uelewa mkubwa zaidi wa seti ya dhana za kisayansi kuliko wanafunzi waliofundishwa kwa Kiingereza. Aidha, Wilmot, (2003) alibaini kwamba, wanafunzi nchini Afrika kusini lugha ya kufundishia inapobadilishwa kutoka Kiingereza kwenda lugha-mama wanafunzi hufahamu mambo mengi zaidi na kujifunza vizuri zaidi pindi wanapofundishwa kwa lugha waliyoizoea. Nao, Heugh na wenzake, (2007) walibaini kwamba, mafanikio yaliyofikiwa ya wanafunzi kufaulu sana kwa masomo ya sayansi na hisabati nchini Ethiopia kati ya mwaka 2000 na 2004 kulionyesha tofauti katika walifundishwa kwa lugha ya wenyeji walifaulu zaidi kuliko wale walifundishwa kwa Kiingereza.

Utafiti mwingine unaofanana na huo wa nchi za nje uliotoa matokeo yanayofanana na hayo ulifanywa nchini Tanzania na wanaisimu mbalimbali kama ifuatavyo:

Mwinsheikhe (2003) wanafunzi wa Elimu ya Sekondari waliofundishwa dhana za kisayansi kwa Kiswahili walielewa zaidi na kufanya vizuri zaidi ya wale walifundishwa kwa Kiingereza. Mwinsheikhe (keshatajwa) anaendelea kudai kwamba, tabia ya kutathmini maarifa ya wanafunzi katika mitihani kwa kutumia lugha wasiyoimudu viwango vya kufaulu haifai kwa kuwa hawana uwezo wa kutumia maarifa hayo baada ya mitihani hiyo.

Aidha, Rubagumya (2003) anadaikwamba, ufundishaji unaotumia lugha inayofahamika baina ya walimu na wanafunzi huleta ufanisi wa kutosha kwasababu wanafunzi watajua jinsi ya kutumia maarifa ya kidhanifu katika taarifa mpya. Rubagumya (keshatajwa) anaenelea kudai kwamba, lugha inapokuwa ni ile iliyozoeleka kwa wanafunzi na ambayo walimu wanaimudu vyema huuleta uelewa mzuri wa dhana ya somo linalofundishwa. Naye, Qorro (1999) anapendekeza kwamba lugha zote mbili zipewe dhima ya kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari. Jambo hili lina ugumu wake katika utekelezaji si rahisi lugha zote zikawa na kazi sawa katika elimu badala yake nikuwachanganya wanafunzi na wafundishaji.

Hivyo basi, tafiti hizo za wanaisimu hapo huu zinabainisha kwamba, nchi nyingi za kiafrika walimu wanatarajiwa kuwafundisha wanafunzi kusoma, kuandika na kupata maarifa katika lugha ambayo, haikuzoeleka kwa wanafunzi na wao wenyewe. Walimu wana ujuzi mdogo wa kutumia kufundishia. Tafiti hizo ni za muda mrefu na hazikutupatia njia za kutatua shida hizo kwa walimu juu ya kuweza kumudu lugha ya kufundishia na ni kipi kifanyike ili wanafunzi wapate maarifa yalikusudiwa katika kiwango cha elimu ya sekondari.

2.1.5 Athari ya Kutotumia Lugha ya Kiswahili Kufundishia Elimu ya Sekondari

Athari ya kutotumika lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya Sekondari ni kubwa sana. Walimu na wanafunzi wanakabiliwa na matatizo makubwa ya mawasiliano.

Kwa mujibu wa World Bank, (2000) vitendo vya ufundishaji wa stadi za mazungumzo salama huzidisha tatizo la mawasiliano na kutojiamini. Wanafunzi

hutoa majibu ya kuitikia, kurudia sentensi au maneno ya mwalimu na kunakili notisi kutoka ubaoni.

Rubagumya (2003) anadai kwamba, mazoezi yanayotegea kufundishwa kwa kukariri mazungumzo salama na kurudia kama kasuku maneno ya mwalimu ni mazoezi yasiyoleta ufanisi wa kutosha, haya wafundishi wanafunzi jinsi ya kutumia maarifa ya kidhanifu katika taarifa mpya.

Macdonald (1990) lugha ya kufundishia nchini Botswana wanafunzi wengi wanaacha shule ama kurudia darasa mwishoni mwa mwaka watano, sababu kuu ni ujuzi mdogo wa lugha ya kufundishia. Alidou na Brock-Utne,(keshatajwa) wanafunzi wanapata kikwazo cha kukosa ujasiri wa kujibu maswali darasani. Alidou na Brock-Utne, (keshatajwa) wanaendelea kudai, wanafunzi wa kike hushiriki kikamilifu darasani kama lugha ya kufundishia ni lugha ya wenyeji.

Kwa mjibu wa Puja (2003) inaonyesha kwamba, ujuzi wa lugha ya kufundishia ni kigezo muhimu cha kufanya vizuri shuleni. Aidha, Macdonald (keshatajwa) inathibitisha kwamba,ujuzi mdogo wa lugha ya kufundishia,ikiwemo ujuzi mdogo wa kusoma,unaathari hasi kwa uwezo wa kufanya vizuri katika masomo yote. Puja (keshatajwa) inadai kwamba, nchini Ujerumani, wanafunzi dhaifu wanatoka kwa familia za wahamiaji ambao nyumbani huzungumza lugha tofauti na ile inayotumiwa shuleni.

Tafiti nyingine zilizofanywa na Mpemba (2007) na Swilla (2009), kuhusu lugha ya kufundishia zinaonyesha kuwa, wanafunzi wa shule za sekondari nchini Tanzania

hawana uwezo wa lugha ya Kiingereza. Udhaifu wa wanafunzi katika lugha hii unasababisha mchakato wa ufundishaji kuwa mgumu.

Watafiti wengi kama vile Mochiwa (1991), Roy Campbell na Qorro (1997), Mkwizu (2002), Malekela (2003), Galabawa na Lwaitama (2004), Senkoro (2004b), wanakubaliana kwamba, matumizi ya lugha ya kigeni katika kufundishia elimu ya sekondari, ina madhara mengi katika utoaji wa elimu kwa ujumla. Miongoni mwa madhara hayo ni kupunguza uwezo wa kutumia lugha kama chombo cha kumwezesha mwanafunzi kung'amua na kueleza mtazamo na hisia zake za ndani, kwa kila kinachomfikia au anachopewa Senkoro (keshatajwa) Watafiti hao (wamaeshatajwa) wanaendelea kueleza kwamba, uwezo huu wa kung'amua na kueleza mtazamo na hisia za ndani kuhusu maarifa ndio msingi wa ubunifu na ugunduzi. Matumizi ya lugha ya kigeni, hupelekea hata walimu kukosa uwezo unaostahili wa kufundisha na wanafunzi kushindwa kuelewa kile anachojifunza.

Utafiti mwingine uliofanywa na Mwinsheikhe (2003) akitaka kujua kama kutumia Kiswahili katika mchakato wa kufundisha na kujifunza kunaweza kuimalisha ushiriki na ufaulu wa wanafunzi kwa masomo ya sayansi. Aligundua kwamba, kuna tatizo la lugha katika kufundisha sayansi. Walimu wengi walikiri kutumia lugha ya Kiswahili wanapofundisha masomo hayo kinyume na sera ya elimu ya Sekondari. Aidha, wanafunzi walisema kwamba, wao wanatumia Kiswahili zaidi katika midala ya masomo yote ya sayansi. Mwinsheikhe (ameshatajwa) anahoji kwamba huo woga wa kuamua kutumia Kiswahili unatoka wapi, wakati Tanzania ilishapata kamusi ya

mwongozo kwa masomo ya Biologia, Kemia na Fizikia tangu 1990 ambayo inaondoa woga kwa pale palipo kuwa na ugumu.

Lugha ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia sekondari imeendelea kuwa na kikwazo kikubwa ambazo kimechangia katika kushindwa kuelewa masomo kwa umakini darasani. Utafiti wa HakiElimu, (2007) ulibaini zaidi ya 60% ya wanafunzi wa sekondari hawajui lugha ya Kiingereza kwa ufanisi na walishindwa kusoma ama kutafsiri aya rahisi ya Kiingereza iliyoandandaliwa kwa ngazi ya darasa la pili. HakiElimu (wameshatajwa) wanaendelea kudai kwamba, huwezi kutarajia mwanafunzi asiyejua Kiingereza kuelewa masomo darasani na hatimaye kufaulu mtihani. Aidha, Missokia na Zombwe (2007) wanadai kwamba, kushuka kwa ufaulu kwenye mitihani ya kidato cha nne mwaka 2010 kumechangiwa na wanafunzi wa shule za kata kutojua lugha ya kufundishia elimu ya Sekondari. Missokia na Zombwe (wameshatajwa) walibaini kuwa walimu wa Sekondari wanapata shida sana kufundisha kwa lugha ya Kiingereza.

Missokia na Zombwe (wameshatajwa) wanaeleza kuwa, lugha ya kufundishia ni muhimu sana kwa wanafunzi na walimu kuweza kuelewa kikamilifu ili kuwawezesha kuwasiliana na kujifunza. Lugha pia inaweza kuwa kikwazo kikubwa cha katika kuchangia kushuka kiwango cha elimu iwapo wanafunzi hawaimudu, maana watahindwa kupokea maarifa kikamilifu na wao kushindwa kujieleza ipasavyo.

Kwa mantiki hiyo ni wazi kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari nchini ina athari kubwa kwa mstakabali wa elimu ya kiwango hicho. Wataalamu hao hapo juu

pamoja na kuwa waligundua kuwa lugha ya kufundishia ina athari hasi ,wameshindwa kutuambia njia za ufumbuzi wa tatizo hilo. Aidha, hatuambiwa nini kinachosababisha walimu wa sekondari kutojua vema lugha ya kufundishia. Tafiti zinazohusiana na ukuaji wa lugha, madhara ya matumizi ya lugha za kigeni katika kufundishia elimu kwa ujumla na tafiti kuhusiana na kwa nini watunga sera hawakipi kipaumbele Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia elimu. Aidha, kama tafiti zinavyoonesha, Kiswahili kimeshakua sana, na kina hadhi kubwa katika ukanda wa Afrika mashariki na kati, na sehemu nyinginezo. Pamoja na ukuaji huo wa lugha ya Kiswahili, hakuna tafiti za siku za karibuni zilizofanywa kuhusiana na haja ya lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari nchini Tanzania. Rubagumya (1990) anahoji kwamba, tunahitaji kujua ni lini Kiswahili kitakuwa lugha rasmi ya kufundishia kiwango cha shule ya sekondari? Tunajua kwamba, wakati Kiswahili kilipotangazwa rasmi kuwa lugha ya kufundishia elimu ya msingi mwaka 1967, lengo lilikuwa ni kukifanya kiwe lugha ya kufundishia elimu ya sekondari ifikapo mwaka 1974.

2.1.6 Changamoto Zinazowakabili Walimu na Wanafunzi Kutokana na Kutotumika kwa Kiswahili katika Ufundishaji wa Elimu ya Sekondari

Changamoto zinazowakabili walimu ni kukosa mawasiliano mazuri darasani, kiasi kinachofanya washindwa kuelewana na wanafunzi hatimaye wanafunzi kushindwa kupata maarifa yalikusudiwa kwa kiwango cha sekondari.

Alidou na Brock-Utne (2005) wanadai kwamba, ujuzi mdogo wa lugha ya kufundishia una athari hasi kwa ufundishaji. Kwa mujibu wa Vinke na wenzake (1998) alibaini kwamba, nchini Netherland walimu wanakabiliwa na changamoto ya

kimawasiliano. Walimu hao hawana ujuzi wa kutosha kutumia lugha ya Kiingereza ambayo ndiyo lugha ya kufundishia. Vinke na wenzake (wameshatajwa) walimu wanauzito wa kutamka na hawana uwezo wa kujieleza kwa kutumia lugha ya Kiingereza wakati wa kufundisha na baada ya vipindi hutumia lugha ya wenyeji zaidi.

Aidha, Wilkinson (2005) anadai kwamba, nchini Uholazi walimu wanashindwa kutumia lugha ya kufundishia kwa mawasiliano mazuri, mara nyingi hubadili msimbo kutoka lugha ya kufundishia ambayo ni Kiingereza kwenda lugha ya wenyeji ili kueleweka vema kile wanachofundisha. Macdonald (1990) alibaini kwamba, nchini Botswana walimu walikuwa na changamoto ya kimawasilino kwa kuwa na ujuzi mdogo wa kutumia lugha ya Kiingereza ambayo ndiyo lugha ya kufundishia elimu ya Sekondari.

Kwa upande wa Tanzania hali ni ngumu kwa walimu kama ilivyo kwa wanafunzi wa shule za sekondari. Kwa mujibu wa Rubagumya (2003) walimu wengi wa shule za sekondari nchini Tanzania hawana uwezo wa kutumia lugha ya Kiingereza kwa ufasaha, kufundishia badala yake huchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza wakati wa kufundisha ili kurahishia ufundishaji.

Wanaisimu hao walifanyia tafiti zao nchi za nje na waliofanyia Tanzania ilikuwa mikoa tofauti na mkoa wa Mwanza. Pia tafiti hizo zinaoneka ni muda mrefu hivyo ni halali kwangu kufanya utafiti huu ili kubaini sababu halisi za sasa zinazo zuia wanafunzi kutopata maarifa ya sekondari.

2.1.7 Mapitio ya Kazi Tangulizi Kisera

Sera ya elimu inayohusu lugha ya kufundishia ndiyo mwongozo wa utayarishaji na utekelezaji wa mpango-lugha katika nchi husika. Maelezo haya yanaungwa mkono na Massamba (2004) kwa kudai kwamba, sera ya lugha ni maelezo rasmi au ya kisheria yanayohusu ukuaji na uendelezaji wa makusudi wa lugha katika jamii fulani ya watu.

Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2011), Sera ni utaratibu wa kuendesha jambo kukidhi haja ya mamlaka na ndani ya sera, ndimo hutamkwa malengo, misingi na michakato ya uteuzi na utekelezaji wa jambo. Hivyo basi, sera ni mwongozo wa kufanya jambo kwa kadri ya mahitaji ya jamii ukibainisha malengo ya jambo linalotakiwa kufanywa, misingi yake na mchakato wa utekelezaji.

Aidha, Sera ya lugha ni jumla ya mawazo, matamko, sheria, kanuni na taratibu zenye kuelezea taratibu za utekelezaji wa mabadiliko ya nafasi na matumizi ya lugha katika jamii. Halikadhalika, sera ya lugha ni matamko au maandishi kuhusu jinsi lugha zinavyopaswa kutumika katika jamii kwa kupeana nafasi ya majukumu katika jamii Massamba na wenzake (2011).

2.1.8 Mambo Yanayochangia Wanafunzi Kukosa Maarifa ya Elimu ya Sekondari Nchini Tanzania

2.1.8.1 Sera ya Lugha ya Kufundishia katika Nchi za Ughaibuni

Uamuzi kuhusu lugha ya kutumia kufundishia ni ya muhimu kwa sababu inaweza kuathiri mbinu na njia ya kufundishia Zhou and Sun (2004), katika mazingira ya Kiingereza kama vile Amerika, lugha ya kufundishia ni Kiingereza. Kila anayehamia

Amerika kutoka nchi nyingine anatakiwa kujifunza lugha ili aweze kuungana na wanafunzi wengine darasani.

Aidha, Zhou and Sun (keshatajwa) anasema kwamba, lugha ya kufundishia katika shule zote za umma nchini Brazil ni kireno cha Brazil. Hata hivyo, lugha ya kufundishia katika Shule nyingine za binafsi ni Kiingereza, kijerumani, kiitaliano au kifaransa. Lugha ya kufundishia nchini Japani ni kijapani kwa viwango vyote vya elimu. Kwa upande wa Israeli, kiebrania ndiyo lugha inayotumiwa kufundishia katika shule nyingi na kiarabu hutumiwa kufundishia shule za waarabu walio wachache. Halikadhalika, August na Shanaha (2006) wanaeleza kwamba, nchini Norwai, lugha ya kufundishia ni Kinorwai na huko Romania lugha ya kufundishia ni kiromania. Pia, nchini Urusi lugha ya kufundishia katika ngazi zote za elimu ni kirusi (August na Shanaha (keshatajwa). Hivyo basi, katika nchi zote hizo hapo juu, lugha za wenyeji ndizo hutumika kufundishia shuleni na katika ngazi zingine za elimu.

Msanjila na wenzake (2000) wanatoa hoja kwamba, lugha za jamii ni bora katika kufundishia kuliko zile za kigeni kwa sababu, kwanza kisaikolojia lugha ya jamii ni mfumo wa alama zenye maana ambazo katika akili ya mwanafunzi hufanya kazi haraka katika kujieleza na kuelewa. Pili, kisaikolojia, lugha ya mtu ni njia ya kujinasibisha na jamii yake na tatu kielimu, mwanafunzi anajifunza haraka Kupitia lugha anayoielewa vema kuliko kujifunza kupitia lugha ya kigeni.

2.1.8.2 Sera ya Lugha ya Kufundishia katika Shule za Afrika

Lugha ya kufundishia katika nchi nyingi barani Afrika ni lugha za ughaibuni kutegemeana na mkoloni aliyeitawala nchi husika. Baadhi ya lugha hizo ni

Kiingereza(kwa nchi zilizokuwa koloni za Mwingereza),kifaransa(kwa nchi zilizokuwa koloni la Mfaransa na Mreno),na kiafrika katika baadhi ya shule za Afrika kusini. Baldauf na Kaplan (2004) wanaeleza kwamba, nchini Rwanda, Kinyarwanda ndiyo lugha ya kufundishia viwango vyote vya elimu.

Kwa mujibu wa Molosiwa na wenzake (1991) lugha ya kufundishia nchini Botswana hutumia Kiingereza, sambamba na kisetswana ambacho ndiyo lugha ya kwanza kwa asilimia themanini ya wananchi. Hali kadhalika, nchini Afrika kusini, lugha ya Kiingereza hutumika kufundishia shuleni ingawa siku za hivi karibuni katiba ya nchi imetambua lugha nyingine za wenyeji.katika nchi ya msumbiji kireno ndiyo lugha ya kufundishia, ingawa marekebisho ya katiba ya mwaka 1990 inakazia kuwa lugha ya taifa iwe lugha ya wenyeji (kibantu).

Pia, Kamwendo (2000) anasema kwamba, sera ya lugha ya kufundishia nchini Malawi ni Kiingereza ingawa Chichewa ndiyo lugha ya taifa inayozungumzwa kwa asilimia hamsini ya wananchi.

Lengo la elimu kwa wote halina maana ikiwa mazingira ya lugha ya kufundishia hayatafanikiwa Brock-Utne (2005).Kwa hali hii basi kuna umuhimu mkubwa kwa nchi za kiafrika kufumbua macho kwa kuthamini lugha zao ili zitumike kufundishia katika viwango vyote vya elimu (Brock-Utne, keshatajwa).

2.1.8.3 Sera ya Lugha ya Kufundishia nchini Tanzania

Mekacha (2000) anasema kwamba, Sera ya lugha nchini Tanzania ni matamko na maagizo ya viongozi yasiyoandikwa, yanayoagiza lugha ipi itumike au isitumike

katika baadhi ya maeneo rasmi ya matumizi ya lugha. Kwa mujibu wa sera ya Elimu na mafunzo(2014),Kiingereza na Kiswahili ni lugha zinazotumika kwa kufundishia na kujifunzia katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Tume ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka (1980), ilipendekeza kwamba Wizara ya Elimu kwa kutumia vyombo vyake, kwa kutumia vyombo vyake, Taasisi ya Ukuzaji wa mitaala, vyuo vikuu kwa ushirikiano na Baraza la Kiswahili la Taifa, ifanye mipango thabiti ya kuziwezesha shule na vyuo vyote nchini kufundisha masomo yote kwa kutumia Kiswahili kuanzia kidato cha kwanza ifikapo mwezi Januari 1985 na Chuo Kikuu kuanzia mwaka 1992. Utekelezaji wa pendekezo hili haukufanywa, badala yake mwaka 1984 Serikali ilitoa tamko linalosisitiza na kuimarisha lugha ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia elimu ya juu. Sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 1995 ilielekeza kuwa lugha ya kufundishia na kutolea mafunzo ya sekondari itakuwa kiingereza. Serikali imetoa Sera ya Utamaduni inayoeleza kusudio lake kwa maneno yatuatayo:

“Mpango maalum wa kuiwezesha elimu na mafunzo katika ngazi zote kutolewa katika lugha ya Kiswahili utaandaliwa na kutekelezwa”
(URT 1977).

Kwa bahati mbaya, Sera hiyo haitaji lini uamuzi huu utaanza kutekelezwa wala hatua za maandalizi ya utekelezaji..

Aidha, Mekacha,(2000), inaelezea kuhusu suala la kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia elimu ya sekondari katika kipindi cha mwaka 1967 mpaka 2000. BAKITA inaeleza mabadiliko ambayo yamekuwa yakitokea katika mtazamo wa serikali kuhusu Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia. Hadi kufikia mwaka 1971,

serikali ilitilia kuwa mkazo azma hiyo itimizwe. Lakini baada ya mwaka huo mkazo ulianza kupungua. Kwa muda mrefu sasa hapa nchini kumekuwa na mabishano ya lugha gani itumike kufundishia mashuleni. Japo tafiti mbalimbali zimethibitisha kwamba Kiswahili kingeweza kuboresha elimu yetu ya sekondari hadi vyuo, bado tumeendelea kung'ang'ania lugha ya mkoloni.

Sera ya elimu (ukurasa wa 52) inataja sababu za Tanzania kuendelea kutumia lugha ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia katika shule za sekondari. Sababu hizo ni kuwawezesha watazania kupata (to access) ujuzi na maarifa, sayansi na teknolojia na kuwasiliana na mataifa mengine. Tujiulize katika mjadala huu iwapo hayo hayawezi kupatikana kwa Kiswahili chetu na hivyo tuendeleo kung'ang'ania Kiingereza ambacho wapo wanaopata shida katika kufundisha kwa Kiingereza. Hatuna mfano wa nchi yoyote katika ulimwengu wa kwanza iliyopata maendeleo ya Sayansi na Teknolojia kwa kutumia lugha ya kigeni.

Hata hivyo, kwa mujibu wa sera ya Elimu na mafunzo (2010), lugha ya Kiswahili, Kiingereza na lugha nyingine za kigeni zinatajwa zifundishwe kama masomo katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Aidha, sera hiyo imekiri kuwa, pamoja na juhudi za kufundisha lugha hizo bado kuna udhaifu wa kumudu lugha sanifu katika mawasiliano.

2.1.9 Athari ya Kutokutumia Lugha ya Kiswahili Kufundishia Elimu ya Sekondari.

Zhou and Sun (2004), katika mazingira ya Kiingereza kama vile Amerika, lugha ya

kufundishia ni Kiingereza. Kila anayehamia Amerika kutoka nchi nyingine anatakiwa kujifunza lugha ili aweze kuungana na wanafunzi wengine darasani.

Kwa mujibu wa Tibategeza (2009), lugha ya kufundishia elimu ya sekondari nchini Tanzania ni Kiingereza Aidha, sera ya elimu inatamka kwamba lugha ya kufundishia elimu ya shule ya sekondari ni Kiingereza (URT 2010).

Aidha, Rubagumya (2003) na Swilla (2009), wanadai kwamba, mfumo wa elimu ya sekondari nchini umeonyesha kuwa ni mfumo wa elimu inayotumia lugha mbili, na umewapa wanafunzi matokeo hasi. Mekacha (2000) kutawala kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli nyingi za kijamii na mawasiliano ya kila siku nchini, Kunachangia katika kupunguza kiwango cha weledi wa lugha ya Kiingereza. Idadi kubwa ya wanaotoa na wanaopata mafunzo ya ngazi ya sekondari hawana weledi wa lugha ya Kiingereza unaotakiwa kulingana na mahitaji ya viwango vyao. Kwahali hyo kuna tatizo ambalo linatakiwa lifanyiwe utafiti. Watafiti wameshindwa kuweka bayana kipi kifanyike ili kuondoa hali inayotumika kufundishia elimu ya sekondari kwa lugha mbili ambayo ni hali inayowapa ugumu walimu na wanafunzi kuchangua lugha ya kutumia kufundishia.

2.1.10 Changamoto Zinazowakabili Walimu Kutokana na Kutotumika Kwa Kiswahili Katika Ufundishaji wa Elimu ya Sekondari

Changamoto zinazowakabili walimu kutokana na kutotumika kwa Kiswahili katika ufundishaji wa elimu ya sekondari ni kutofuata sera ya elimu kuhusu lugha ya kufundishia elimu ya sekondari. Maelezo hayo yanaungwa mkono na wanaisimu wafuatao:

Gorham na Ruberg (1985) anadai kwamba, sera ya lugha kufundishia nchini Angola ni kireno, ingawa walimu huchanganya na lugha za wenyeji wakati kufundisha darasani. Hali hii ni changamoto kubwa kwa walimu wa nchini humo, kwasababu itakuwa vigumu kufafanua dhana kamili ya somo kama inavyotakiwa. Pia inaonekana sera ya elimu nchini Angola haifutwi kikamilifu.

Halikadhalika katika nchi ya Afrika ya kati hali inafanana na ilivyo chini Angola. McIntyre (1985) anadai kwamba, sera ya elimu nchini humo inatamka kuwa lugha ya kufundishia ni Kifaransa. Angola. McIntyre (keshatajwa) anasema kwamba, walimu nchini humo wanakumbwa na changamoto za mawasilino darasani. Walimu wanatumia kifaransa na Kisango ambayo ni lugha ya wenyeji, kwa hali hiyo basi ya sera ya elimu haifutwi na badala yake inavurugwa.

Kwa upande wa Tanzania, Sera ya elimu na Mafunzo (2014) inataja kwamba Lugha ya Kiingereza hutumika kufundishia katika shule za sekondari. Kwa mujibu wa Swilla (2009), mfumo wa elimu ya sekondari nchini umeonyesha kuwa ni mfumo wa elimu inayotumia lugha mbili ambazo ni Kingereza na Kiswahili. Mekacha (2000) Idadi kubwa ya wanaotoa mafunzo ya ngazi ya sekondari hawana weledi wa lugha ya Kiingereza unaotakiwa kulingana na mahitaji ya viwango vyao, hulazimika kuchanganya lugha mbili darasani.

Hali hii inachangia kushusha kiwango cha elimu nchini Tanzania na changamoto kubwa kwa walimu, kwasababu itakuwa vigumu kwa mwalimu kumaliza mada zilizo kwa muhtasari ikiwa atatumia lugha mbili. Kuna umuhimu wa kuendelea kufanya

utafiti huu ili kubaini zaidi kipi chanzo cha changamoto hizo ili kuona kama zinaweza kutafutiwa ufumbuzi ili kuondoa tabia hiyo iliyo kinyume cha sera ya elimu nchini.

2.2 Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ni mawazo ama mwongozo unasaidia kuelezea jambo fulani. Maelezo hayo yanakubaliana na yale ya Massamba, (2004) anaye dai kwamba, nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kiolezo cha kuelezea jambo. Halikadhalika, TUKI (2004) wanaunga mkono maana hiyo kwa kusema kwamba, nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani.

Kiunzi cha nadharia ambacho kimetumika katika utafiti huu utaongozwa na nadharia ya uzamaji au kujitosa (Immersion). Nadharia hii ilibuka katika miaka ya 1960 na kukubalika katika nchi nyingi duniani kama njia ya kueleza mipango ya mabadiliko ya lugha ya kufundishia shuleni. Ilianzishwa na mwanasaikolojia wa Canada Dkt. Wallance E. Lambert 1960 aliyekuwa mkuu wa kitengo cha Saikolojia katika Chuo Kikuu cha Mc GILL. Katika mwaka 1965 kundi la wazazi lililojiita “*St. Lambert Bilingual School Study group*” lilianzisha harakati za kudai kuanzishwa kwa mpango wa elimu ya Uzamaji katika Kifaransa kwa ajili ya watoto wao walio kulia katika jamii ya lugha ya Kiingereza ili kurekebisha kasoro za lugha ya watoto wao (Lambert, 1960)..

2.3 Nadharia ya Uzamaji

Kwa mujibu wa Skutnabb-Kangas na McCarty (2008) uzamaji ni utaratibu wa

kurekebisha kasoro za watoto wanaopelekwa shule zenye lugha mbili. Kwamba mpango huu hulenga kuimalisha lugha ya wachache na kuendeleza lugha yao ya nyumbani. Kwa upande wa Tanzania, lugha ya Kiswahili ni lugha ya nyumbani kwa walio wengi, inatakiwa ipewe mikakati ya kuiendeleza kupitia mfumo wa elimu ya Sekondari ambazo zimeenea nchi nzima.

Naye Lambert (1984) anatoa hoja kwamba, elimu ya Utosaji huwakilisha mfumo wa elimu wenye utaratibu uliopangiliwa zaidi kufundishia wanafunzi kupitia lugha ya pili ya wachache. Bostwick (1999) anatoa mifano ya nchi za Singapore, Switzerland, India, Canada na nchi nyingi za Afrika kuwa ni mifano michache ya nchi zinazotambua lugha mbili za taifa. Kwa kawaida lugha hizi hutumika katika uwanja wa shughuli za kisiasa, kiofisi na kijamii.

Aidha, Johnson na Swain (1997) wanapendekeza kuwa, mtaala wa utosaji unatakiwa uwe sambamba na mtaala wa lugha ya kwanza ya mahali. Kwamba, mpango wa kuongeza wa lugha mbili kwa wanafunzi uwe ni kuongeza ujuzi wa lugha ya pili wanapoendelea kukuza lugha yao ya kwanza na pia utamaduni wa darasa uwe ni jamiilugha ya mahali. Kwa upande wa Tanzania lugha ya Kiswahili ni ya kwanza kwa baadhi na ya pili kwa wengine. Kwa hiyo kuna umuhimu mkubwa wa kutumia lugha ya Kiswahili darasani na lugha ya kigeni kuwa ya kuongeza ujuzi wa mwanafunzi kimataifa.

Vilevile, May (2008) anadai kwamba, mkazo mkuu wa elimu ya uzamaji ni kuendeleza mwanafunzi kuwa na uwezo wa kuzungumza lugha ya kufundishia na kumpa maarifa ya kitaaluma.

Naye Cummins (2008) anatoa hoja kwamba, dhana ya uzamaji linatumika kwa mitazamo miwili tofauti katika muktadha wa elimu: Kwanza ni utaratibu wa mfumo wa kupanga elimu inayofundishwa kwa lugha mbili ambapo wanafunzi huzaamishwa katika mazingira ya kujifunza lugha mbili. Lugha ya kwanza ya kufundishia kwa kawaida huanza kwa mwaka wa kwanza au wapili wa mwanzoni mwa mpango wa masomo. Pili ni uingizaji wa wahamiaji au watoto wa jamiilugha ndogo katika mazingira ya darasa ambalo hutumia lugha yao ya pili au ya tatu ambayo ni ya jamiilugha kubwa. Kusudi lake ni kustawisha ustadi au umahili katika lugha ya kufundishia.

Hivyo, katika utafiti huu, nadharia ya uzamaji au Utosaji ilitumika kwa kuzingatia maana ya pili ambapo wahamiaji na wananchi wachache hutumia ya Kiswahili kama lugha ya pili, kutokana na mazingira yaliyowakuza.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inashughulika na mbinu mbalimbali ambazo zimetumika katika mchakato wa kufanya utafiti. Sura hii imegawanyika katika sehemu nane. Sehemu ya kwanza imejadili usanifu wa utafiti. Sehemu ya pili imejadili eneo la utafiti na sababu za kuteua eneo hilo. Sehemu ya tatu imejadili usampulishaji kwa kuangalia aina ya walengwa waliotafitiwa. Sehemu ya nne imejadili jinsi mtafiti alivyo pata sampuli. Sehemu ya tano imejadili mbinu mbalimbali zilizotumiwa na mtafiti katika kukusanya data. Sehemu ya sita imejadili maadili ya utafiti kwa kuangalia haki za mtafitiwa. Sehemu ya saba inaeleza kwa ufupi jinsi data zilivyochambuliwa, majadiliano na matokeo ya majadiliano. Sehemu ya nane inatoa muhtasari wa sura nzima.

3.2 Mkabala wa Utafiti

Mkabala wa utafiti huu ni wa maelezo. Mkabala wa maelezo kama ulivyofafanuliwa na Punch, (2004) ni kupanga, kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoielezwa na walengwa wa utafiti. Mtafiti huzipanga kutokana na maudhui au makundi yanayofanana. Mtafiti alikuwa makini katika kueleza, kufafanua, kuhakiki, kuvumbua, kufanya majaribio, kutafsiri taarifa alizozipata kupitia muundo huu wa utafiti. Sehemu ndogo ya utafiti imetumia takwimu kama kielelezo.

3.3 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza. Mkoa wa Mwanza

umegawanywa katika wilaya za kiutawala saba (07) ambazo huunda wilaya saba (07) za kielimu ziiwazo Ilemela, Magu, Misungwi, Kwimba, Nyamagana, Sengerema na Ukerewe. Wilaya mbili ziiwazo Ilemela na Nyamagana ziko ndani ya jiji la Mwanza hivyo huunda halimashauri za manispaa mbili za jiji la Mwanza. Halmashauri ya manispaa ya Ilemela imepakana na Sengerema kwa upande wa magharibi, Magu kwa upande wa mashariki, Ukerewe kwa upande wa kaskazini na Nyamagana kwa upande wa kusini. Makao makuu ya halmashauri ya manispaa ya Ilemela ni Buswelu.



Kielezo 3.1: Ramani ya jiji la Mwanza kuonyesha mahali ilipo wilaya ya Ilemela

Chanzo: Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza 2015

Aidha, utafiti huu unahusu walimu wa wilaya ya Ilemela katika mkoa wa Mwanza tu kwa kuwakilisha maeneo mengine ya Tanzania yenye mazingira yanayofanana na mazingira ya wilaya ya Ilemela. Wilaya hii ilichaguliwa kwa sababu inagawanyika katika sehemu kuu mbili, za mjini na vijijini. Hivyo basi, taarifa zilizokusanywa pamoja na matokeo ya utafiti huo zilitegemewa kutoa taswira ya hali halisi ya maeneo yote ya mjini na vijijini. Sababu ya pili ya kuchagua wilaya hii ni kwamba, wilaya hii haipo mbali na eneo analotoka mtafiti, na kwa hiyo, ilikuwa rahisi kuufanya utafiti huo.

Kielelezo namba 3.1 hapo juu kinaonyesha mahali ilipo halmashauli ya wilaya ya Ilemela katika jiji la Mwanza.

3.4 Sampuli na Usampulishaji

3.4.1 Sampuli

Sampuli ni kundi dogo la watu au vitu vinavyo teuliwa na mtafiti kkuwakilisha kundi kubwa.

Kwa mujibu wa Mligo,(2012) sampuli ni kundi fulani la watu au vitu lililoko ndani ya mkusanyiko wa watu au vitu ambao mtafiti anaamini kwamba linazo habari zitakazomwezesha kujibu swali lake la utafiti. Kuchagua sampuli ni kuchagua kundi dogo la watu au vitu katika mkusanyiko wenye makundi ya aina nyingi kwa malengo maalumu aliyonayo mtafiti kwa ajili ya utafiti wake. Kwa kuwa si rahisi kwa mtafiti kuwatafiti watu wanaoishi eneo la wilaya ya Ilemela, mtafiti alifanya uteuzi wa sampuli ili kupata kundi dogo la watu waliofanyiwa utafiti kuwakilisha kundi kubwa. Walengwa wa utafiti ni watu au vitu vyenye tabia, desturi na sifa zinazofanana.

Kwa mujibu wa Koul (2009) walengwa ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Kwa hiyo, katika Utafiti huu kundi lengwa walikuwa wanafunzi na walimu wa shule tano za Sekondari ambazo ni: Sekondari ya Kiloleli, Sekondari ya Ibingilo, Sekondari ya Nyamanoro, Sekondari ya Kitangiri na Sekondari ya Pasiansi wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza.

Utafiti huu uliwahusisha walimu wa shule tano za sekondari na wanafunzi wa kidato cha kwanza mpaka cha nne kutoka shule hizo.

Mtafiti alichagua walengwa hawa kwa sababu walimu waliotafitiwa wanauzoefu wa kufundisha elimu ya sekondari kwa muda mrefu hivyo walitegemewa na mtafiti kuwa watatoa majibu kuhusu changamoto zinazowakabili wanapofundisha darasani kwa kutumia lugha ya kigeni.

Sababu nyingine ya mtafiti kuchagua shule hizo ni kwamba, shule hizo ni kongwe. Kwa mfano shule ya sekondari Kitangiri ilianzishwa mwaka 1998, hivyo mtafiti aliamini kuwa shule hizo zitatoa majibu yahasuyo mada ya utafiti huu kutokana na uzoefu wake kwa lugha ya kufundishia na matokeo ya mitihani ya miaka mingi.

Aidha, shule za sekondari lengwa zina uzoefu wa matokeo ya taifa ya kidato cha nne kama tulivyo onyesha matokeo ya shule mbili kati ya tano lengwa, hivyo walimu na wanafunzi walisaidia kutoa majibu kulingana na mada ya utafiti huu Takwimu ya

Matokeo ya kidato cha nne ya shule za sekondari pasiansi na Ibungilo kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2012 mpaka 2014 kwa masomo ya Kiswahili, Jogografia na Historia inathibitisha kwamba Kiswahili kinaongoza kwa kiwango cha ufaulu. Katika utafiti huu shule ya sekondari Pasiansi itawakilishwa na alama A na Ibungilo alama B. Mgawo wa viwango vya alama umefuata kanuni ifuatayo kwa matokeo ya kidato cha nne mwaka 2012 ya shule A: A=5, B=4, C=3, D=2, F=1 pamoja na idadi ya wanafunzi 206 kwa somo la Kiswahili, 228 kwa Historia, 222 kwa Jogografia wastani wajumla ya alama za Kiswahili 1.6, Historia 1.2, Jogografia 1.3.

Aidha, matokeo ya mwaka 2012 ya shule B; Idadi ya wanafunzi kwa somo la Kiswahili walikuwa 162, Historia 178 na Jogografia 179, wastani wa jumla ya alama kwa Kiswahili 1.8, Jogografia 1.5 na Historia 1.4. Hii inaonyesha kwamba, Kiswahili kilikuwa na matokeo mazuri kikifuatwa na Jogografia na mwisho Historia. Kwahiyo wanafunzi wanaelewa zaidi somo linalofundishwa kwa Kiswahili kuliko linalofundishwa kwa Kiingereza. Chukua idadi ya wanafunzi (IW), jumla ya alama (JA) na wastani wa alama (WA) kwa kila somo. Jedwali namba 1.3.1 hapo chini linathibitisha takwimu hiyo

Jedwali 3.1: Takwimu ya Matokeo ya Kidato cha Nne 2012 Shule A na B

Matokeo ya kidato cha nne, 2012 ya shule A								
SOMO	A	B	C	D	F	IW	JA	WA
KIWAHILI	0	1	18	90	97	206	335	1.6
HISTOIA	0	0	9	37	182	228	283	1.2
JOGORAFIA	0	1	10	54	157	222	299	1.3
Matokeo ya kidato cha nne, 2012 ya shule B								
SOMO	A	B	C	D	F	IW	JA	WA
KISWAHILI	0	0	36	65	61	162	299	1.8
HISTORIA	0	2	15	44	117	178	258	1.4
JOGRAFIA	0	0	21	49	109	179	268	1.5

Chanzo: Utafiti wa mwaka, 2015

Mgawo wa viwango vya alama umefuata kanuni ifuatayo kwa matokeo ya kidato cha nne mwaka 2013 mpaka 2014: A=7, B+=6, B =5 C=4, D=3, E=2, F=1 pamoja na idadi ya wanafunzi 184 kwa somo la Kiswahili, 186 kwa Historian 164 kwa Jografia wastani wajumla ya alama za Kiswahili 3.2, Historia 1.5, Jografia 2.2. Aidha, matokeo ya mwaka 2013 ya shule B yanabainishwa kwa kutumia kanuni iliyotumiwa hapo juu. Idadi ya wanafunzi kwa somo la Kiswahili walikuwa 170, Historia 175 na Jografia 170, wastani wa jumla ya alama kwa Kiswahili 3.6, Jografia 2.5 na Historia 1.8. Hii inaonyesha kwamba, Kiswahili kilikuwa na matokeo mazuri kikifuatwa na Jografia na mwisho Historia. Hivyo basi, wanafunzi wanaelewa zaidi somo linalofundishwa kwa Kiswahili kuliko linalofundishwa kwa Kiingereza. Jedwali namba 1.3.2 hapo chini linathibitisha takwimu hiyo.

Jedwali 3.2: Takwimu ya Matokeo ya Mwaka, 2013 kwa Shule A na B

Matokeo ya kidato cha nne, 2013 ya shule A										
SOMO	A	B+	B	C	D	E	F	IW	JA	WA
KIWAHILI	0	9	17	50	45	53	10	184	590	3.2
HISTORIA	0	0	3	18	35	48	82	186	288	1.5
JOGRAFIA	0	0	5	23	43	29	64	164	368	2.2
Matokeo ya kidato cha nne, 2013 ya shule B										
SOMO	A	B+	B	C	D	E	F	IW	JA	WA
KIWAHILI	0	9	41	48	42	18	12	170	625	3.6
HISTORIA	0	1	18	40	37	47	32	175	493	1.8
JOGRAFIA	0	1	9	30	52	35	43	170	440	2.5

Chanzo: Utafiti wa mwaka, 2015

Matokeo ya kidato cha nne 2014 yabainishwa kwa kufuata mgawo ufuatao: A=7, B+=6, B =5 C=4, D=3, E=2, F=1 pamoja na idadi ya wanafunzi 128 kwa somo la Kiswahili, 131 kwa Historian 126 kwa Jografia wastani wajumla ya alama za

Kiswahili 3.3, Historia 2.7, Jografia 2.7. Hii inaonyesha kwamba, Kiswahili kilikuwa na matokeo mazuri, Jografia na Historia yalilingana kwa wastani wa matokeo hayo.

Aidha, matokeo ya mwaka 2014 ya shule B yanabainishwa kwa kutumia kanuni iliyotumiwa hapo juu. Idadi ya wanafunzi kwa somo la Kiswahili walikuwa 142, Historia 140 na Jografia 142, wastani wa jumla ya alama kwa Kiswahili 4.0, Jografia 3.1 na Historia 3.0. Hii inaonyesha kwamba, Kiswahili kilikuwa na matokeo mazuri kikifuatiwa na Jografia na mwisho Historia. Hivyo basi, wanafunzi wanaelewa zaidi somo linalofundishwa kwa Kiswahili kuliko linalofundishwa kwa Kiingereza. Jedwali namba 1.3.3 hapo chini linathibitisha takwimu hiyo.

Jedwali 3.4.3. Takwimu ya matokeo ya mwaka 2014 kwa shule A na B

Matokeo ya kidato cha nne, 2014 ya shule A										
SOMO	A	B+	B	C	D	E	F	IW	JA	WA
KIWAHILI	0	3	12	47	26	36	4	128	420	3.3
HISTORIA	0	4	14	27	11	49	26	131	359	2.7
JOGRAFIA	0	7	9	25	14	44	27	126	344	2.7
Matokeo ya kidato cha nne, 2014 ya shule B										
SOMO	A	B+	B	C	D	E	F	IW	JA	WA
KIWAHILI	0	9	38	60	20	14	1	142	573	4.0
HISTORIA	0	4	16	38	18	55	9	140	429	3.0
JOGRAFIA	0	5	17	39	20	54	7	142	446	3.1

Chanzo: Utafiti wa mwaka, 2015

Takwimu ya matokeo iliyo hapo juu inaonyesha kuwa masomo yanayofundishwa kwa lugha ya Kiingereza hayafahamiki kwa wanafunzi na hatimaye hushindwa kuyafaulu kwenye mitihani hiyo ni dalili ya kukosa umilisi kwa lugha hiyo na hawapati maarifa yalikusudiwa kwa usahihi. Aidha, takwimu hiyo inathibitisha kwamba, Kiswahili kinafahamika vizuri na kinafaa kupewa jukumu la kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari nchini

Takwimu hiyo pia, inaonyesha kuwa kuna tatizo lugha ya kufundishia elimu ya sekondari, masomo yanayofundishwa kwa lugha ya Kiingereza hayafahamiki kwa wanafunzi na hatimaye wanashindwa kuyafaulu mitihani. Hiyo ni dalili ya kwamba, hawapati maarifa yalikusudiwa kwa usahihi kwa kiwango hicho cha sekondari. Pia shule hizo zinaonyesha kuwa na uzoefu wa matokeo ya mitihani ya kidato cha nne kwa muda mrefu.

Watafitiwa walitoka katika shule tano (5) za sekondari kati ya shule arobaini na nane (48) za wilaya ya Ilemela zenye wanafunzi wa jinsia zote mbili. Shule hizo zilipewa majina ya shule A, B, C, D na shule E. Kila shule ilitoa walimu watano wa masomo ya sanaa.

Vile vile walimu wawili walitoka katika kundi la walimu wa sayansi: mmoja wa kike na mmoja wa kiume. Mwalimu mmoja alitoka katika kundi la utawala, ambao ni mkuu wa shule au makamu wake. Hivyo, kulikuwa na sampuli ya walimu 25 toka katika hizo shule tano. Aidha, kila shule ilitoa sampuli ya wanafunzi 16, kila kidato kilitoa wanafunzi 4, wa jinsia zote mbili. Hivyo, kufanya sampuli ya wanafunzi kuwa ni 80 kati ya wanafunzi 30,482 wa wilaya ya Ilemela. Kwa hiyo, utafiti ulifanywa kwa kutumia sampuli ya watu 105. Aidha, sampuli katika utafiti huu ilikuwa ni asilimia 14 ya watafitiwa wote, walimu na wanafunzi. kwa mujibu wa Kothari, (2012) anadai kwamba, kiasi hicho cha sampuli kinatosha kuwakilisha kundi zima la watafitiwa; na taarifa yake ikajumuishwa kwa kundi zima la watafitiwa. Wilaya hii ina shule za sekondari 48 katika kata 09 ambao ni Ilemela, Buswelu, Nyakato, Kitangiri, Nyamanoro. Pasiansi, Kirumba, Bugogwa, Sangabuye (Shule 24 zikiwa za

serikali na 24 zikiwa za watu binafsi na mashirika ya dini zenye jumla ya walimu 888 na wanafunzi 30,482).Wanafunzi walio wengi wamesajiliwa katika shule za sekondari za serikali.Utafiti huu umehusisha shule tano (05) tu katika shule za serikali.Aidha, utafiti ulijikita katika kidato cha kwanza (1) hadi nne (4) tu.

Jedwali 3.5. Shule Zilizofanyiwa Utafiti (Idadi Ya Walimu na Wanafunzi).

Shule Za Serikali

Shule	Walimu			Wanafunzi		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Kiloleli	17	28	45	431	418	849
Ibungilo	18	24	42	373	441	814
Nyamanoro	23	22	45	397	414	811
Kitangiri	25	24	49	324	290	614
Pasiansi	16	10	26	421	414	835
JUMLA	99	108	207	1946	1977	3923

Chanzo: Utafiti wa uwandani: 2015

Utafiti huu ulifanywa katika wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza. Sababu zilizomfanya mtafiti achague eneo hili ni kutokana na ukweli kwamba wakazi wake wamegawanyika sehemu kuu mbili: nusu mjini na nusu nyingine iko vijijini, hivyo taarifa zilizopatikana katika wilaya hii zinawakilisha mitazamo ya mazingira yote mawili: mazingira ya mijini na mazingira ya vijijini. Pia mtafiti amechagua eneo hili kwa sababu ni rahisi kufikika, hata pale ambapo alihitaji taarifa za ziada wakati utafiti ulipokuwa unaendelea.

Aidha,wilaya hii ni mpya na hakuna utafiti wowote ulikwisha fanyika katika eneo hili kuhisiana na lugha ya kufundishia elimu ya sekondari.Kwahali hiyo basi,hili

lilikuwa eneo sahihi ya kufanyia utafiti kwa kuwa husisha walimu na wanafunzi ambao ndiyo wahanga wa kutotumiwa kwa lugha ya Kiswahili katika kufundishia elimu ya sekondari.

3.4.2 Usampulishaji

Usampulishaji kama ulivyouelezwa na Kothari (2004) ni mpango wa kuchangua sampuli maalum kutoka kundi kubwa. Zipo aina mbili za usampulishaji zilizotwazo usampulishaji wa kinasibu na usampulishaji usio wa kinasibu (Kombo na Tromp 2006). Aidha, usampulishaji ni namna ya kupata kundi dogo linalopatikana kuwakilisha kundi kubwa la watu au vitu kisha kutoa taarifa ya utafiti zinazohusu kundi la mahali pa utafiti Bryman (2008) anasema kwamba, usampulishaji ni idadi ndogo ya kufanyiwa utafiti utakapochagua wachache kutoka katika kundi kubwa. Koul (2009) anafafanua kuwa, usampulishaji nasibu ni njia rahisi katika usampulishaji na kila kitu katika vitu au vikundi hupewa nafasi sawa ya kuchaguliwa. Anaendelea kusema kwamba, usampulishaji nasibu linganishi ni usampulishaji unaoweza kutumiwa pale unapowagawa watafitiwa kwa kugawa watu kwa uwiano sawa.

Katika utafiti huu tumetumia aina zote mbili za usampulishaji kwa sababu zilituwezesha kupata data zilizoweza kutoa majibu ya jumla katika sampuli kubwa. Tulitumia Usampulishaji usio wa kinasibu kwa sababu utafiti wetu ulilenga makundi maalum ya sampuli. Kwa mfano, kundi la walimu wa kidato cha kwanza hadi cha nne, Wakuu wa shule na wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne tu.

Tulitumia usampulishaji wa kinasibu kwa sababu utafiti wetu ulifanyika katika shule ambazo ziliteuliwa kwa kupanga orodha ya shule zote za sekondari za halmashauri ya wilaya ya Ilemela kwa kufuata alfabeti, kisha kuchukua shule tano kutoka kwenye orodha ya shule zote kila baada ya shule tano kwenye orodha kutoka ya kwanza hadi ya mwisho. Katika utafiti huu, shule tano kati ya arobaini na nane zilipatikana kwa njia ya usampulishaji wa kinasibu. Majina ya shule zote yaliandikwa kwenye kadi maalumu kwa ajili ya usampulishaji. Kadi hizo zilichanganywa na kisha kuokotwa kadi tano kwa njia ya unasibu.

Vile vile, katika kila shule, zilitengenezwa kadi zenye majina ya walimu wa masomo ya sanaa pekee yao na majina ya walimu wa masomo ya sayansi pekee yao. Kwa kutumia mbinu ya kinasibu walichaguliwa walimu wawili toka katika kila kundi: kundi la walimu wa masomo ya sanaa na kundi la walimu wa masomo ya sayansi. Walimu wakuu au makamu wao walichaguliwa kwa mujibu wa madaraka yao. Kila darasa, walitenganishwa katika makundi makuu mawili: wanafunzi wa kike na wa kiume. Halafu, wanafunzi wawili walichaguliwa toka katika kila kundi kwa kutumia mbinu za kinasibu ili kupata sampuli nasibu linganishi ya sampuli ya jumla ya wanafunzi.

3.5 Mbinu za Kukusanya Data

Katika utafiti huu mbinu tatu za kukusanya data zilitumika. Data ni kila taarifa yoyote inayokusudiwa katika utafiti. Taarifa hiyo inaweza kuwa maneno, picha, vitu mbalimbali na chochote kile kitakachosaidia kupata taarifa ya utafiti. Kwa mujibu wa Enon (1995) data ni taarifa zilizokusanywa, zilizochunguzwa au kubuniwa kwa

madhumuniya kuchanganuliwa katika hatua za utafiti wa awali. Utafiti huu ulitumia njia data msingi na data upili.

Kothari (2012) anasema kwamba, data msingi ni zile taarifa zilizokusanywa uwandani ambazo zinatafutwa na mtafiti mwenyewe, kwa njia ya kuuliza maswali (hojaji), maswali ya dodoso, na kwa kudadisi. Kwa upande mwingine, data upili ni data unazozipata kwa kusoma ripoti mbalimbali, majarida mbalimbali, magazeti, makala mbalimbali na vyanzo vingine vya kupata taarifa kama vile tafiti zilizotangulia.

Aidha, mbinu za kukusanya data, kama anavyoeleza Pons (1992) ni vielelezo vinavyokubalika ambavyo vinathibitisha ukweli wa matokeo. Data za msingi (awali) kama anavyozieleza Kothari (2004) ni zile data ambazo hukusanywa kwa mara ya kwanza uwandani. Data hizi zimekusanywa wakati mtafiti yuko uwandani. Data hizi ndizo na zimejibu maswali ya utafiti. Data hizi zilikuwa zimechambuliwa kwenye madaftari zilitumika kwa ajili ya kurekodi taarifa. Kothari (2004) anaeleza kuwa, data za upili ni zile ambazo tayari zilishakusanywa na zimeshatumika na kuhifadhiwa.

Data hizi pia mtafiti alizipata kupitia maandiko ya wataalamu mbalimbali pamoja na ripoti za aina tofauti. Taarifa hizi pia zilikusanywa kwa kuangalia kazi zilizopita kuhusiana na mada kwakuangalia vitabu, majarida na machapisho mbalimbali katika maktaba kuu ya mkoa wa Mwanza na maktaba ya Chuo Kikuu cha Mount Meru Mwanza Tanzania na kwenye mitandao ambayo inahusu lugha ya kufundishia.

Katika utafiti huu mbinu tatu zilitumika katika kukusanya data ni mahaojiano, hojaji na maktaba. Data nyingine zilipatikana katika tovuti. Pia data zilizokusanywa zilikuwa za kiidadi na kimaelezo.

Kwa kuwa mtafiti mwenyewe ndiye mwenye ujuzi, uelewa wa namna ya kuhoji wahojiwa na kukusanya data pamoja na uelewa wa maadili ya utafiti, basi data za utafiti huu zilikusanywa na mtafiti mwenyewe katika maeneo yote yaliyokuwa yamechaguliwa kufanyia utafiti.

3.5.1 Mbinu ya Maktabani

Utafiti huu utatumia mbinu au njia ya maktabani ili kuweza kukusanya data kuhusu haja ya kutumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia elimu ya sekondari. Kwa hiyo Utafiti huu utafanyika katika maktaba ya chuo kikuu cha Mount Meru, maktaba ya mkoa wa Mwanza na maktaba ya nyumbani ili kusoma na kurejea machapisho ya wataalamu wa lugha.

3.5.2 Mbinu ya Hojaji

Kwa mujibu wa Kothari (2012) mbinu ya hojaji ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti anaandaa maswali au dodoso yake yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani. Halikadhalika, Kothari (keshatajwa) Maswali haya yanaweza kuhitaji majibu mafupi au marefu kutegemeana na taarifa inayohitajika na mtu anayepewa dodoso hizo. Mbinu hii ni ya kutumia maswali yaliyoandikwa kwa lengo la kujibiwa na mtafitiwa. Kwa mujibu wa TATAKI (2013), hojaji ni karatsi yenye maswali ya uchunguzi. Aidha, Mligo (2012) anaendaendelea kudai kwamba, hojaji ni karatasi iliyoandikwa

maswali ambayo hupewa mtafitiwa ili aandike majibu. Mtafitiwa anapokea karatasi ya hojaji anatakiwa asome maswali yaliyomo, ayaelewe na kuyatafsiri na kisha atoe majibu kulingana na jinsi alivyoulizwa. Kwa ujumla njia ya hojaji, data hukusanywa kutokana na mtafitiwa kujibu maswali yaliyoorodheshwa katika karatasi. Karatasi zenye maswali hugawiwa kwa watafitiwa ili waweze kuzijaza na hatimaye mtafiti kupata taarifa muhimu za kiuchunguzi.

Mbinu hii ilitumiwa ili kusaidia katika kukusanya data ambazo mtafiti aliamini zitapatikana kutoka kwa walengwa. Dodoso zilitumika kutafuta data toka katika malengo yote mahususi. Maswali yaliyofungwa yaliulizwa sambamba na maswali huru kwa lengo la kutomfunga mtafitiwa kutoa majibu ya mlengo mmoja. Mtafiti aliwagawia maswali ya hojaji watafitiwa 105:Walimu 25 na wanafunzi 80 wa shule ya sekondari tano (05) za wilaya ya Ilemela.Walimu walitakiwa kujibu maswali 12 wakati wanafunzi walitakiwa kujibu maswali 8. Karatasi zote za dodoso zilijibiwa na kukunywa na mtafiti ambaye alikwenda moja kwa moja kwenye shule husika na kungojea kujazwa kwa karatasi zote za kila shule.Dodoso zote zilimtaka mtafitiwa kujibu maswali ya kueleza, “ndiyo” na “hapana” na kuweka alama ya “vema” kwenye jibu sahihi.Rejea maswali katika kiambatanisho.

3.5.3 Mbinu ya Mahojiano

Kothari (2004) anasema kwamba, njia ya mahojiano hujumuisha uwasilishaji wa mdomo, ana kwa ana baina ya mtafiti na mtafitiwa. Anaendelea kudai kwamba, mahojiano ni njia ambayo hutumiwa na mtafiti kwa kufuata utaratibu wa kutafuta majibu ya maswali yaliyopangwa kwa wahojiwa.

Kwa upande mwingine Mligo (2012) anadai kwamba, mahojiano ni njia ambayo mtafiti huweza kuitumia katika utafiti kwa maeneo halisi waishio watu, habari nyingi ambazo hazijulikani hupatikana kutokana na mwingine au kundi moja la watu na kundi lingine.

Kwa mujibu wa Mligo (keshatajwa) kuna aina tatu za mahojiano, ambazo ni mahojiano yaliyo huru. Aina hii ya mahojiano hutoa uhuru kwa mhoji kuuliza maswali ya ziada ili kupata majibu yaliyo sahihi zaidi. Mhojiwa anakuwa na uhuru wa kujibu kwa kueleza na kufafanua zaidi kwa mawazo yake kuhusiana na swali aliloulizwa, pia anaweza kuuliza Swahili pale ambapo hajaelewa. Aina ya pili ni mahojiano yasiyo huru. Mahojiano hufuata aina moja tu ya maswali kwa watu wote wanaohojiwa na huwa na muundo wa aina mmoja tu wa kuhoji. Aina ya tatu ni mahojiano ya nusu huru na nusu yamefungwa Mlingo (keshatajwa). Aina hii humpa nafasi mtafiti kuuliza maswali yaliyofungwa na kufuatilia kwa undani jibu lililotolewa na mhojiwa.

Katika kazi hii mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano huru, kwa sababu mahojiano huru hutoa uhuru wa mtafiti na mtafitiwa kuuliza swali lolote kulingana na mahali au kitu chochote anachotaka kujua kwa wakati huo. Aidha, muundo wa namna ya kuendesha mahojiano huweza kubadilika badilika kufuatana na mtu anayehojiwa na mahali ambapo mahojiano hayo hufanyika.

Katika utafiti huu, mahojiano yalitumika kwa wanafunzi 80 na walimu 25 wa shule za sekondari tano zinazomilikiwa na serikali. Lengo la kutumia mbinu ya mahojiano

ni kulinganisha majibu yaliyopatikana kwa mbinu ya hojaji kupitia maswali dodoso ili kutafuta usahihi wa data zenyewe.

3.6 Vyanzo vya Data

Utafiti utatumia aina mbili za data. Ambapo mtafiti atatumia data za msingi ambazo ni zile data atazozipata kutoka kwa watafitiwa na data upili ni data ambazo atazipata kutoka maktabani kupitia vitabu na matini mbalimbali vya wataalamu wa lugha.

3.6.1 Data za Msingi

Kombo na Trombo (2006) wanasema kwamba data za msingi ni data zinazopatikana kutoka kwenye sampuli ya Utafiti au watafitiwa. Pia ni data zinazopatikana kutokana na maswali, mahojiano, vikundi vya majadiliano, kuonana ana kwa ana na hata njia ya majaribio. Na data hizo ndio sababu ya kupatikana kwa data upili. Utafiti huu utatumia data za msingi ambazo mtafiti atazipata kutoka kwa watafitiwa kupitia mahojiano ya ana kwa ana na kupitia dodoso kutoka kwa watafitiwa juu ya haja ya kutumia Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari.

3.6.2 Data Upili

Kwa mujibu wa Kothari (2004) data upili ni taarifa ambazo tayari zilishakusanywa na watu wengine. Katika ukusanyaji wa data, mtafiti atapata data hizi kutoka maktabani kupitia vitabu, majarida, magazeti na makala mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti huu. Aidha, Kothari (keshatajwa) anaendelea kusema kwamba, data upili zinaweza kuwa zimechapwa katika machapisho, vitabu, magazeti na matini.

3.7 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ulifanywa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo (Qualitative) na kiidadi (Quantitative) kutegemea aina ya tatizo na asili ya data iliyokusanywa. Mbinu hizi zinastahili kwa sababu zilitoa maelezo na kutoa ufafanuzi kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kufundishia elimu ya Sekondari. Data ubora/stahilivu zilibadilishwa ili kupata data kiasi kwa lengo la kufanya urahisi wa usiwalishwaji na upimaji wake kwa njia mbalimbali kama vile njia ya majedwali na asilimia, ambazo ni njia rahisi kueleweka kwa mtumiaji wa utafiti.

3.8 Maadili ya Utafiti

Maadili ni mahusiano yaliyomo kati ya wanajamii katika maisha yao ya kawaida kwa kufuata kanuni zilizowekwa na kukubaliwa na wanajamii hao zitumike kuongoza maisha yao. Mligo (2012) anaunga mkono kauli hii kwamba, maadili ni kanuni zilizowekwa na kukubaliwa na jamii ili zitumike kuongoza mwenendo wa maisha na tabia halisi ya maisha ya mwanajamii husika.

Pons (1992), maadili ya utafiti ni pamoja na haki ya kuwa na usiri yaani matafiti hatatoa siri ya mtafitiwa. Pia ameeleza haki ya mtafitiwa kuhakishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni ya utafiti, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swali atakalopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti. Mtafiti ametambua haki haki zote hizi na kuzitekeleza. Tatizo lolote litakalotokea itakuwa ni juu ya mtafiti mwenyewe.

Kwa kuwa utafiti huu una madhumuni ya taaluma tu na si vinginevyo, maadili ya utafiti yalizingatiwa ili kuepuka migogoro ya baadaye utafiti huu umepukwa kutoa

siri za mtafitiwa kwa kuandika jina na kile alichochangia kwa kusema na kwa kuandika.

3.9 Hitimisho

Sura hii imejadili vipengele mbalimbali ambavyo vinahusiana na mbinu ya utafiti. Vipengele vilivyo husika ni eneo la utafiti wahusika lengwa ambao walikuwa ni walimu ishirini na watano na wanafunzi themanini walioteuliwa kutoka kwenye shule teule. Vilevile kipengele cha sampuli na usamplishaji zilijadiliwa kwa mapana yake. Kipengele hiki kilihusisha sampuli ya shule tano. Aidha, mbinu mbili zilitumika wakati wa kukusanya data ambazo zilikuwa ni hojaji na mahojiano. Maadili ya utafiti, ukusanyaji na uchambuzi wa data pia yameelezwa kwa ufupi.

SURA YA NNE

4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo yaliyopatikana kutokana na utafiti wa uwandani na maktabani na pia kuchambua na kujadilia data na matokeo ya utafiti. Uwasilishaji wa data na majadala wa matokeo umefanyika kwa kutumia misingi na kanuni za kiunzi cha nadharia ya lugha ya kufundishia ya uzamaji au utosaji. Uwasilishaji na majadiliano juu ya matokeo hayo umelenga kujibu maswali ya utafiti yaliyokusudiwa ili kukamilisha malengo mahususi ya utafiti. Aidha, sura hii inawasilisha matokeo na kuyajadili kwa mujibu wa data iliyochambuliwa na hoja mbalimbali za wanazuoni kama zilivyo kwenye mapitio ya kazi tangulizi katika tasnifu hii.

Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu kama ifuatavyo: Sehemu ya kwanza inawasilisha data na matokeo ya lengo mahususi namba moja. Sehemu ya pili inawasilisha na kujadili data za matokeo ya lengo mahususi. Sehemu ya tatu inawasilisha na kujadili data na matokeo lengo mahususi la tatu.

Uwasilishaji na Uchambuzi wa data yamehusisha malengo mahususi ya Utafiti huu na kujibu maswali ya utafiti. Baada ya kuyawasilisha matokeo ya utafiti katika kila kipengele kwa kuhusisha na nadharia mbalimbali kiisimu na hoja za wanazuoni mbalimbali katika mapitio ya kazi zilizopita na hali halisi katika maisha ya kila siku kwa kuzingatia malengo.

Utafiti huu umehusisha shule tano (05) tu katika shule za serikali. Aidha, utafiti ulijikita katika kidato cha kwanza (1) hadi nne (4) tu. Jumla ya wanafunzi waliotafiwa ilikuwa 80 na walimu 25. Shule 05 za sekondari zilikusika, ambazo ni Kitangiri, Nyamanoro, Pasiansi, Ibungilo na Kiloleli ambazo ziko katika Wilaya ya Ilemela mkoani mwanza.

4.2 Mambo yanayochangia Wanafunzi Kukosa Maarifa ya Elimu ya Sekondari

Sehemu hii inawasilisha matokeo na kujadili kwa kuzingatia mambo yanayochangia wanafunzi kukosa maarifa ya elimu ya sekondari. Aidha, sehemu hii imejikita katika kujadili hoja zinazohusiana na lengo la kwanza la utafiti huu.

4.2.1 Kiswahili Kutotumika Kufundishia Elimu ya Sekondari Tanzania

Mtafiti alitumia hoja kwa njia ya maswali dodoso kuwauliza walimu kama Kiswahili kutotumika kufundishia elimu ya sekondari yaweza kuwa moja ya mambo yanayochangia wanafunzi kukosa maarifa ya elimu ya sekondari. Kutokana na majibu ya swali dodoso hili yalionyesha kuwa asilimia 64% (16) ya walimu walionyesha kwamba kutotumika kwa lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari ndiyo sababu mojawapo ya wanafunzi wa sekondari kukosa maarifa ya elimu ya hiyo. Kwa upande mwingine asilimia 28% (07) ya Walimu hao walikanusha kuwa hiyo siyo sababu. Hata hivyo, asilimia 8% (02) ya walimu hao hawakuonyesha mwelekeo wowote kuhusu swali hili. Jedwali namba 4.2 linadhahirisha matokeo haya.

Mtafiti aliwauliza wanafunzi pia kama kutoeleweka vizuri lugha ya Kiingereza katika shule za sekondari kunachangia kukosa maarifa ya elimu ya sekondari. Kutokana na majibu ya wanafunzi juu ya swali hili yalionyesha kuwa asilimia 97.5% (78) ya wanafunzi wote 80 walikubali kuwa hiyo ndiyo sababu mojawapo kubwa ya kukosa kwao maarifa ya elimu ya sekondari. Asilimia ndogo sana 2.5% (02) ya wanafunzi hao ndiyo hawakuonyesha mwelekeo wowote kuhusu swali hili. Jedwali namba 4.2 linadhirisha haya matokeo.

Jedwali: 4.2. Majibu ya Walimu na Wanafunzi Juu ya Mambo Yanayochangia Wanafunzi Kukosa Maarifa ya Elimu ya Sekondari

A		Maswali ya Dodoso kwa Waalimu			
Na.	Mambo yanayochangia wanafunzi kukosa maarifa ya elimu ya sekondari ni pamoja na haya yafuatayo:	Majibu			
		Ndiyo	Hapana	Sijui	Jumla
		% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi
1	Kiswahili kutokutumika kufundishia elimu ya sekondari	64%(16)	28%(7)	8%(2)	100%(25)
2	Kiswahili kutopewa umuhimu wa kutumika kufundishia elimu ya Sekondari	56%(14)	44%(11)	00%(0)	100%(25)
3	Kutoeleweka vizuri Lugha ya Kiingereza katika shule za sekondari	72%(18)	28%(07)	00%(0)	100%(25)
B		Maswali Dodoso kwa Wanafunzi			
Na.	Mambo yanayochangia wanafunzi kukosa maarifa ya elimu ya sekondari ni pamoja na haya yafuatayo:	Majibu			
		Ndiyo	Hapana	Sijui	Jumla
		% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi
1	Kutoeleweka vizuri Lugha ya Kiingereza katika shule za sekondari	97.5%(78)	00%(0)	2.5%(02)	100%(80)

Chanzo: Utafiti wa uwandani (2015)

Matokeo haya yanaashiria kwamba walimu wengi (64%) wanapata shida ya lugha ya kufundishia elimu ya sekondari kwa kiswahili. Aidha, matokeo haya yanaashiria kuwa, kutokana na kushindwa kwa walimu hawa kufundishia vema kwa lugha wasiyoilewa vema, hakuna mawasiliano fanisi baina yao na wanafunzi darasani. Kwa sababu hiyo baadhi ya wanafunzi wanashindwa kupata maarifa ya kutosha ya elimu ya sekondari.

Kwa mujibu wa Senkoro (2004) lugha huwezesha ufundishaji na lugha inayotumiwa kufundishia darasani inatakiwa iwe lugha inayoeleweka vizuri kwa walimu na wanafunzi. Prah (2004) anaongeza kwamba, lugha ya kufundishia ndiyo inayotumika kujenga mfumo wa elimu na ndiyo lugha inayotumiwa kuwasilisha stadi na maarifa ya msingi ya umma kuimarisha ubunifu na kuendeleza maarifa ya wajifunzaji. Kwa mitazamo hiyo ya wataalamu, lugha ya kufundishia inapaswa kuwa lugha inayoeleweka vema kwa ufasaha kwa walimu na wanafunzi ili kuwezesha kueleweka vizuri maarifa mapya yanayofundishwa.

Matokeo ya utafiti huu yanaashiria kuwa hoja hii haizingatiwi katika ufundishaji wa elimu ya sekondari wilayani Ilemela. Kutokana na hali hiyo, wanafunzi wa sekondari katika wilaya hii hawapati vema maarifa yanayokusudiwa kwa ajili yao. Hii inadhihirishwa na majibu yalitolewa na walimu 64% (16) walikiri kwamba wanafunzi hawaelewi wanachofundishwa na baadhi ya walimu pia hawana uwezo wa kuzungumzo kwa ufasaha lugha ya kufundishia elimu ya sekondari. Asilimia 28% (07) walikanusha kuwa hiyo siyo kweli bali ni uzembe wa wanafunzi wenyewe kwa kukosa umakini wakati asilimia 8% (2) walikosa mwelekeo.

Msanjila na wenzake (2011) wanasema kwamba, matumizi ya lugha sahihi katika kufundishia masomo katika mfumo wa elimu ni zaidi ya kuwasaidia wanaojifunza kwa sababu huendeleza pia vipaji vyao, na kubwa zaidi lugha hiyo huendelezwa ili kukabili mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Tafsiri yake ni kwamba, kutotumia ya lugha ya kiswahili kufundishia elimu ya Tanzania hakuwasaidii wanafunzi kufikia malengo yao. Aidha, hakuwasaidii kuendeleza sawasawa vipaji na ubunifu wa wanafunzi na hakuikuzi lugha ya Kiswahili ili iendane na wakati na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

4.2.2 Kiswahili Kutopewa Umuhimu wa Kutumika Kufundishia Elimu ya Sekondari

Mtafiti vilevile alitumia hojaji kwa njia ya maswali dodoso kuwauliza walimu kama Kiswahili kutopewa umuhimu wa kutumika kufundishia elimu ya sekondari yanaweza kuwa moja ya mambo yanayochangia wanafunzi kukosa maarifa ya elimu ya sekondari. Matokeo kutokana na majibu ya swali dodoso hili yalionyesha kwamba asilimia 56% (14) ya walimu 25 walionyesha kwamba Kiswahili kutopewa umuhimu wa kutumika kufundishia elimu ya sekondari ndiyo sababu mojawapo ya wanafunzi wa sekondari kukosa maarifa ya elimu ya hiyo. Kwa upande mwingine asilimia 44% (11) ya Walimu hao walikanusha kuwa hiyo siyo sababu

Jedwali namba 4.1 linadhihirisha haya matokeo. Mtafiti aliwauliza wanafunzi pia kama kutoeleweka vizuri lugha ya Kiingereza katika shule za na kuchangia kukosa kwao maarifa ya elimu ya sekondari. Matokeo kutokana na majibu ya wanafunzi juu ya swali dodoso hili yalionyesha kuwa asilimia 97% (78) ya wanafunzi wote 80

walikubali kuwa hiyo ndiyo sababu mojawapo kubwa ya kukosa kwao maarifa ya elimu ya sekondari. Aidha, asilimia ndogo sana 2.5% (02) ya wanafunzi hao ndiyo hawakuonyesha mwelekeo wowote kuhusu swali hili. Jedwali namba 4.1 linadhirisha haya matokeo.

4.2.3 Kutoeleweka Vizuri Lugha ya Kiingereza katika Shule za Sekondari

Mtafiti aliwauliza wanafunzi pia kutoeleweka vizuri. Lugha ya Kiingereza katika shule za sekondari kunachangia kukosa kwao maarifa ya elimu ya sekondari. Matokeo kutokana na majibu ya wanafunzi juu ya swali dodoso hili yalionyesha kuwa asilimia 97.5% (78) ya wanafunzi wote 80 walikubali kuwa hiyo ni sababu mojawapo kubwa ya kukosa kwao maarifa ya elimu ya sekondari. Aidha, asilimia ndogo sana 2.5% (02) ya wanafunzi hao ndiyo hawakuonyesha mwelekeo wowote kuhusu swali hili. Jedwali namba 4.2 linadhihirisha haya matokeo.

Swali hilo liliulizwa pia kwa walimu, matokeo yanaashiria kwamba walimu asilimia 72% (18) ya walimu walikiri kwamba, hawamudu vema kutumia lugha ya Kiingereza kaufundishia masomo ya sekondari. Jibu hili linakubaliana na jibu la swali la kwanza lililoonyesha kuwa walimu wengi wanapata shida ya lugha wasipofundishia elimu ya sekondari kwa Kiswahili. Majibu ya asilimia 28% (7) walikanusha. Aidha, matokeo haya yanaashiria kuwa kutokana na kushindwa kwa walimu hawa kufundisha vema kwa lugha wasiyoielewa vizuri hakuna mawasiliano fanisi baina yao na wanafunzi darasani. Hoja hii inadhihirishwa na matokeo ya majibu ya wanafunzi wote (97.5%) kutoeleweka vizuri kwa lugha ya Kiingereza

katika shule ya sekondari kunachangia wao kutokupata maarifa ya elimu ya sekondari.

Matokeo hayo yaashiria kuwa kutokueleweka vizuri lugha ya Kiingereza katika shule za sekondari ni moja ya sababu ya baadhi ya wanafunzi kushindwa kupata maarifa ya kutosha ya elimu ya sekondari. Matokeo haya yanakubalina na Peterson (2006) ambaye anayesema kuwa, wanafunzi wana mawazo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili. Wanafunzi hawa wanaelewa zaidi wanapofundishwa katika lugha ya Kiswahili ambayo wanaitumia hata nje ya darasa na katika maisha yao ya kila siku, wanapofundishwa kwa lugha hiyo wanapata maarifa kamili kuliko wanapofundishwa kwa Kiingereza. Lugha yenye ufanisi na ya kuleta matokeo yanayotakiwa ni ile tu inayofahamika vizuri kwa walimu na wanafunzi. Peterson (keshatajwa) anaendelea kudai kwamba, kufundishia lugha isiyofahamika kwa wanafunzi kunachangia kuharibu ubora wa elimu kwa kuwa wanafunzi hawaelewi kile kinachofundishwa.

Naye, Qorro (2006) anaunga mkono hoja hiyo kwa kusema, pale wanafunzi wanaposhindwa kuongea lugha ya kufundishia hakika hawataweza kupata maarifa. Ugunduzi huu unakubaliana na ugunduzi wa watafiti wengine kama vile akina Qorro (2005) anayesema kwamba, Kiswahili kinapaswa kutumiwa katika nyanja zote za mawasiliano ya kitaifa, na hasa katika elimu. Anaendelea kusema kwamba, nchi nyingi duniani ambazo hutumia lugha zake hupata mafanikio makubwa katika Nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Naye Rubagumya (2003) anayesema kwamba, wanafunzi wa Tanzania wanaelewa walimu wao vizuri wakati ule ambapo mafunzo yanatolewa kwa lugha ya Kiswahili.

Hivyo basi, wanafunzi wa shule za sekondari katika wilaya ya Ilemela hawapati maarifa ya sahihi kwa kuwa lugha inayotumiwa na walimu kufundishia haifahamiki vizuri.

4.2.4 Data Zilizotokana na Mahojiano.

Mtafiti aliwahoji walimu 25 na wanafunzi 80 kutoka katika shule tano za sekondari kuhusu kama iko haja ya kuendelea kutolewa kwa lugha ya kigeni. Matokeo ya mahojiano hayo yalionyesha kuwa asilimia 84% (21) ya walimu 25 na 97.5% (78) walipendekeza kwamba, elimu ya sekondari ifundishwe kwa Kiswahili. Sababu ya kwanza iliyotolewa katika hoja hii ni kwamba, Kiswahili ndiyo lugha mama ya mtanzania ya mawasiliano. Kwa mfano, mwalimu mmoja alisema:

“Lugha ya Kiswahili inafahamika vizuri kwa sababu ni lugha mama (mother tongue) , na baadhi ni lugha yao ya pili (second language) ya watoto walio wengi, wanauwezo wa kuizungumzia na kuiandika vizuri. Lakini pia, ni lugha wanayoitumia kila siku katika Nyanja zote za maisha yao ya kawaida”.

Hoja ya mwalimu huyu inathibitisha kwamba walimu wanapata shida kufundishia lugha ambayo wanafunzi wao hawaiwi na hivyo kushindwa kupata maarifa ya kiwango cha sekondari. Pia, wanafunzi wengi wanadai kuwa kuna haja ya elimu ya sekondari kutolewa kwa lugha ya Kiswahili kwa hoja kwamba ndiyo lugha wanayoiongea tangu utotoni. Ni lugha waliyoizoea, wanayoifahamu vizuri, ni lugha inayowawezesha kujieleza vizuri kuliko lugha ya Kiingereza.

Sababu nyingine kubwa iliyotolewa na wahojiwa wengi ni kwamba, hata kama maagizo na maandiko ya kisera mbalimbali kuhusu lugha ya kufundishia elimu ya

sekondari yanasomeka hivyo, lakini kiuhalisia lugha ya Kiswahili bado hutumika kufundishia elimu ya sekondari isivyo halali, walimu wengi hutumia lugha mchanganyiko, Kiingereza na kiswahili kwa wakati mmoja ili wanafunzi waelewe vizuri. Hoja hii inathibitishwa na jibu la mwalimu mmoja aliyesema hivi;

“Hakuna haja ya kuendelea kutumia lugha ya kigeni kwa sababu, baadhi ya walimu hawana msingi na uwezo mzuri wa lugha ya Kiingereza. Kwa wanafunzi, ni tatizo zaidi. Kuna haja gani ya kuendelea kutumia lugha ambayo inawatatiza hata wenyewe? Kinachofanyika madarasani ni kwamba, walimu hutumia Kiingereza na Kiswahili kufundishia ili wanafunzi wao waelewe. Ikiwa walimu hao hutumia Kiswahili ili kuwafanya wanafunzi wake waelewe, kwa nini basi Kiswahili kisihalalishwe moja kwa moja kuwa ni lugha ya kufundishia?”

Sababu kubwa ya tatu iliyotolewa katika lengo la kwanza ni kwamba, Kiswahili kimeshakua kwa kiwango cha kukiwezesha kuwa lugha ya kufundishia. Haya yanathibitishwa na mwalimu mmoja aliyesema hivi;

“Taarifa tunazosikia mara kwa mara katika vyombo vya habari zinaonyesha kwamba, sasa hivi Kiswahili kimekua sana. Nasikia hata umoja wa mataifa, achilia mbali Afrika mashariki, wanakusudia kukifanya Kiswahili kuwa ni mojawapo ya lugha ya ulimwengu. Kama hayo ni kweli, ni vema sisi wenyewe tukakithamini na kukifanya kiwe lugha ya kufundishia elimu ya sekondari.

4.2.5 Majumuisho ya Lengo la Kwanza la Utafiti

Uchambuzi wa data katika lengo la kwanza la utafiti unaonyesha kwamba. Kipengele hiki kilihusu lengo mahsusi la utafiti namba 1 tu ambalo ni mambo yanayochangia wanafunzi kukosa maarifa ya elimu ya sekondari. Mtafiti alihitaji kuwasilisha matokeo ya utafiti kwa njia ya data juu ya swali la utafiti lililoegemea kwenye lengo la kwanza la utafiti. Uchambuzi ulibaini kuwa kutotumika kwa lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari kuna changia wanafunzi kukosa maarifa ya kiwango

hicho. Walimu na wanafunzi hawana ujuzi wa kutosha kutumia lugha ya Kiingereza kama wanavyo tumia vizuri lugha ya Kiswahili. Majibu hayo yanafanana na mawazo ya Massamba na wenzake (2009) wanaodai kuwa, lugha ya Kiswahili ni lugha ambayo hutumiwa na watu ambao idadi yake yakadiriwa kuwa zaidi ya milioni 60. Idadi hiyo imekadiriwa kwa kuzingatia kwamba lugha hii inazungumzwa na takribani kila mtu katika Tanzania.

Kwa mujibu wa mahojiano, wahojiwa wengi wanapendelea elimu ya sekondari ingetumiwa kwa lugha ya Kiswahili. Sababu ya kwanza iliyotolewa katika hoja hii ni kwamba, Kiswahili ndiyo lugha mama ya mtanzania ya mawasiliano. Kwa mfano, mwalimu mmoja anasema hivi;

“Lugha hiyo (yaani lugha ya Kiswahili) hiyo inafahamika vizuri kwa sababu wengi wao ni lugha mama (mother tongue language), na baadhi ni lugha yao ya pili (second language acquisition). Kwa watoto wengi, wanauwezo wa kuzungumza na kuiandika vizuri. Lakini pia, ni lugha wanayoitumia kila siku katika Nyanja zote za maisha yao ya kawaida”.

Pia, wanafunzi wengi wanaona haja ya elimu ya sekondari kutolewa kwa lugha ya Kiswahili kwa madai kwamba ndiyo lugha waliyokua nayo tangu utoto wao, ni lugha waliyoizoea, wanayoifahamu vizuri, ni lugha inayowawezesha kujieleza vizuri kuliko lugha ya Kiingereza. Hayo yanathibitishwa na mfano mmoja wa mwanafunzi aliyesema hivi,

“Nilitaka kuacha shule wakati naanza kusoma form one. Yaani ilikuwa kila nikiingia darasani, walimu wanafundisha kwa Kiingereza tu utafikiri hawajui kama sisi hatujui Kiingereza. Mbaya zaidi, ukiulizwa swali, wanataka ujibu kwa Kiingereza. Sasa mimi sijui Kiingereza, najibuje kwa Kiingereza? Kama isingekuwa ushauri wa wazazi wangu, ningeacha shule. Kwa hiyo, mimi napendekeza elimu ya sekondari itolewe kwa lugha ya Kiswahili. Kama hawataki tufundishwe kwa Kiswahili, basi kwanza watufundishe Kiingereza mwaka mzima mpaka tukijue ndipo tuanze kufundishwa masomo mengine”

Matokeo ya utafiki huu yanaonyesha kwamba, ili kupata ufumbuzi wa tatizo la wanafunzi kukosa maarifa ya kiwango cha elimu ya sekondari, inatakiwa yafanyike mambo yafuatayo:

- i) Kiswahili kipewe dhima ya kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari
- ii) Kiswahili kipewe umuhimu wa kwanza wa kutumika kufundishia elimu ya sekondari ili kujenga msingi imara wa wanafunzi
- iii) Kuongeza bidii ya kutafsiri machapisho na vitabu ili viendane na hitaji la elimu ya sekondari la kuwapa maarifa wanafunzi kwa kutumia lugha wanayoielewa vizuri

Matokeo haya yanaenda sambamba na mawazo ya Msanjila na wenzake (2009) wanaosema kwamba, kuingizwa kwa Kiswahili katika mifumo ya kompyuta kunazidi kuongeza haja ya kukifanya Kiswahili kiwe ni lugha iliyojitosheleza kufundishia ngazi zote za elimu. Wanaendelea kusema kwamba, mafanikio hayo kwa jamii yanakiweka Kiswahili katika nafasi nzuri ya kupewa nafasi ya kutumika katika elimu ya sekondari kama zilivyopewa hizo lugha kubwa zilizopiga hatua kisayansi na kiteknolojia, na kwamba nafasi hiyo itaipa lugha ya Kiswahili fursa mpya ya kuweza kutumika pia kujenga maendeleo ya jamii kwenye misingi ya utamaduni wa jamii ya Tanzania.

4.3 Athari ya Kutokutumika Kwa Lugha ya Kiswahili Kufundishia Elimu ya Sekondari

Mtafiti alitumia hojaji ya maswali dodoso kuwauliza walimu kama kuna athari ya kutotumika kwa lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari. Kutokana na

majibu ya swali dodoso hili yanaonyesha kuwa asilimia 92%(23) ya walimu walionyesha kwamba kutotumika kwa lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari kuna athari za kutofundishia lugha ya kiswahili. Aidha, asilimia 8%(02) ya walimu walikanusha kuwa hakuna athari.

Jedwali: 4.3: Matokeo ya Walimu na Wanafunzi Kuhusu Athari ya Kutokutumika kwa Lugha ya Kiswahili Kufundishia Elimu ya Sekondari

A					
Maswali ya Dodoso kwa Waalimu					
Na.	Moja ya mambo yafuatayo ni athari mojawapo ya kutokutumika kwa lugha ya kiswahili kufundishia elimu ya sekondari	Majibu			
		Ndiyo	Hapana	Sijui	Jumla
		% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi
1	Kushuka kwa ubora wa elimu kitaaluma	92%(23)	8%(2)	(0)0%	100%
2	Matumizi ya lugha zaidi ya moja wakati wa kufundisha	88%(22)	12%(3)	(0)0%	100 %
3	Walimu wengi kupata changamoto katika kutumia lugha ya kigeni	96%(24)	4%(1)	(0)0%	100%
4	Mada mbalimbali kutokwisha kwa wakati	92%(23)	8%(2)	(0) 0%	100 %
5	Somo kutoeleweka kwa urahisi	92%	8% (2)	(0)0%	100%
B					
Maswali ya Dodoso kwa Wanafunzi					
Na.	Athari ya kutokutumika kwa lugha ya kiswahili kufundishia elimu ya sekondari	Majibu			
		Ndiyo	Hapana	Sijui	Jumla
		% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi
1	Kushuka kwa ubora wa elimu kitaaluma	90%(72)	10%(8)	(0)0%	100%
2	wanafunzi kushindwa kumudu taaluma,	90%(72)	10%(8)	(0)0%	100%
3	kutofaulu mtihani kwa viwango stahiki	96.25%(77)	2.5%(2)	(0)0%	100 %
4	kushindwa kuchangia mada darasani,	97.5%(78)	2.5%(2)	(0)0%	100%
5	adhabu za kuongea Kiswahili shuleni	97.5%(78)	2.5%(2)	(0)0%	100 %

Chanzo: Utafiti wa uwandani: 2015

Mtafiti aliwauliza wanafunzi pia kama kuna athari za kutokutumika kwa lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari. Majibu yalioletwa na wanafunzi

yalionesha kuwa, asilimia 97.5% (78) ya wanafunzi walikiri kwamba wanapata athari hasi kwa kutofundishwa kwa lugha ya Kiswahili wakati asilimia 2.5% (2) walikanusha kuwa hakuna athari kwa kutofundishwa kwa Kiswahili Jedwali namba 4.2 inadhihirisha haya matokeo.

Matokeo katika jedwali namba 4.2 hapo juu yanaashiria kwamba, walimu wanapata athari kwa kutofundishia kiswahili katika shule za sekondari. Athari hizo ni Kushuka kwa ubora wa elimu kitaaluma, wanafunzi kushindwa kutumia uwezo na ujuzi wa kubuni na kung'amua mambo yanayowakabili baada ya kumaliza elimu ya sekondari, vikwazo vya mawasiliano dhidi ya walimu na wanafunzi, matumizi lugha zaidi ya moja wakati wa kufundisha, walimu wengi kupata changamoto katika kutumia lugha ya kigeni, mada mbalimbali kutokwisha kwa wakati, Somo kutoeleweka kwa urahisi, wanafunzi kutoshiriki vizuri katika kujibu maswali darasani na Wanafunzi kukosa uwezo wa kujibu vizuri maswali ya kujieleza.

Kwa upande wa wanafunzi, matokeo ya utafiti huu yanaashiria kuwa suala la athari zitokanazo na elimu ya sekondari kutofundishwa kwa Kiswahili, halizingatiwi katika ufundishaji wa elimu wilayani Ilemela. Kutokana na hali hiyo, wanafunzi wa sekondari katika wilaya hii hawapati maarifa ya kutosha ya kiwango cha elimu ya sekondari. Badala yake ni kupata athari nyingi zitokanazo na elimu ya sekondari kutofundishwa kwa lugha Kiswahili.

Hii inadhihirishwa na majibu yalitolewa na wanafunzi 97.5% walikiri kwamba, wanafunzi wanapata athari nyingi za kutofundishwa kwa lugha ya Kiswahili wakati asilimia 2.5% walikanusha.

Asilimia 90% ya wanafunzi hao walitaja athari hizo kuwa ni pamoja na wanafunzi kushindwa kumudu taaluma, asilimia 97.5% yao walitaja athari ya kutofaulu mtihani kwa viwango stahiki, asilimia 97.5% kushindwa kuchangia mada darasani na asilimia 2.5 walikanusha, asilimia 97.5% adhabu za kuongea Kiswahili shuleni asilimia 97.5 walikiri na asilimia 2.5 walikanusha, migogoro na wazazi kwakuwa adhabu hutolewa baada ya vipindi na kama wakati wa vipindi mwanafunzi hukosa kuhudhuria baadhi ya vipindi hivyo matokeo yake ni kushindwa kufaulu mitihani yao.

Athari nyingine ni wanafunzi kutoelewa vizuri wanayofundishwa asilimia 90% na hivyo kutoboea katika fani husika kwa vile huwalazimu wanafunzi wengi kusoma kwa kukariri. Wanafunzi kukosa umahiri wa kujieleza juu ya jambo wanalolielewa wakati huo wasilimia 10% ya wanafunzi walikanusha.

Kwa mujibu wa Rubagumya (2003), wanafunzi wanawaelewa vizuri walimu wa shule za sekondari pale ambapo mafunzo hutolewa kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, Mpemba (2007) na Swilla (2009), wanadai kuwa walimu wengi wa Tanzania hawana umilisi wa kutosha wa lugha ya Kiingereza udhaifu huu katika lugha ya Kiingereza huwasababisha walimu kupata ugumu katika kufundisha masomo ya elimu ya sekondari kwa ufanisi, hivyo kusabisha wanafunzi kutopata maarifa ya kutosha yaliyokusudiwa kwa ajili yao. Hii inamaanisha kuwa walimu wengi wa Tanzania wanamudu vizuri lugha ya Kiswahili kuliko Kiingereza, hali hii inaashiria kuwa lugha ya Kiswahili ingefaa zaidi kufundishia elimu ya sekondari badaa ya lugha ya Kiingereza inayotumika sasa hivi.

4.3.1 Ufumbuzi wa athari za Kutofundishia Lugha ya Kiswahili

Katika kuchunguza ufumbuzi wa athari za kutofundishia lugha ya Kiswahili, wahojiwa walitakiwa kujibu katika dodoso lililomtaka mhojiwa kutoa mapendekezo ya suluhisho la athari zilizotokana na kujibu swali la tano, sita na saba. Data zilizopatikana zinaonyesha kwamba, asilimia 64 % (16) ya walimu 25 walipendelea Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia, asilimia 12% walipendelea Kiingereza kiwe ndiyo lugha ya kufundishia wakati 24 % (16) walisema hawajui ufumbuzi wa athari hizo. Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa ufumbuzi wa athari hizo unategemea mambo yafuatayo kufanyika; matoe

- i) Kiswahili kipewe kipaumbele kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari ili kuwapa urahisi walimu na wanafunzi kuwasiliana na kuelewa masomo wanayofundishwa
- ii) Lugha ya Kiingereza ifundishwe kama somo kwa ajili ya kuwasaidia wajifunzaji kuwa na ufahamu wa kuwasiliana kimataifa.

Mtafiti aliwauliza wanafunzi pia kama kuna namna inavyotakiwa ifanyike ili kuleta ufumbuzi kwa athari walizobainisha. Mtokeo kutokana na majibu ya wanafunzi juu ya Swahili hili yalionyesha kuwa asilimia 72.5% (58) walipendelea Kiswahili kipewe kipaumbele, wakati asilimia 17.5% (14) ya wanafunzi walipendelea Kiingereza kipewe kipaumbele na asilimia 10% (8) walishindwa kuwa na mwelekeo wowote kuhusu swali hili. Jedwali 4.3 linadhahirisha haya matokeo.

Data za matokeo ya utafiti huu katika jedwali namba 4.3 zinaashiria kwamba, walimu asilimia 64% wanapendelea elimu ya sekondari ifundishwe kwa lugha ya

Kiswahili ili kuweka mawasiliano mazuri baina yao na wanafunzi. Aidha, matokeo yanashiria kuwa asilimia 72.5% ya wanafunzi wanapendelea zaidi lugha ya Kiswahili iwe ndiyo kufundishia elimu ya sekondari.

Jedwali: 4.4: Maoni ya Walimu na Wanafunzi juu Ufumbuzi wa athari za Kutofundishia Elimu ya Sekondari kwa Lugha ya Kiswahili

A Maswali ya Dodoso kwa Waalimu					
Na.	Ufumbuzi wa athari za Kutofundishia Lugha ya Kiswahili	Majibu			
		Ndiyo	Hapana	Sijui	Jumla
		% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi
1	Kiswahili kipewe kipaumbele kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari	64%(16)	12%(3)	24%(6)	100%
2	Lugha ya Kiingereza ifundishwe kama somo kwa ajili ya kuwasaidia wajifunzaji kuwa na ufahamu wa kuwasiliana kimataifa.	64%(16)	24%(6)	12%(3)	100 %
B Maswali ya Dodoso kwa Wanafunzi					
Na.	Ufumbuzi wa athari za Kutofundishia Lugha ya Kiswahili	Majibu			
		Ndiyo	Hapana	Sijui	Jumla
		% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi
1	Kiswahili kipewe kipaumbele kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari	72.5%(58)	17.5%(14)	10%(8)	100%
2	Lugha ya Kiingereza ifundishwe kama somo kwa ajili ya kuwasaidia wajifunzaji kuwa na ufahamu wa kuwasiliana kimataifa.	72.5%(58)	17.5%(14)	10%(8)	100 %

Chanzo: Utafiti wa uwandani: 2015

Kwa upande mwingine, matokeo ya utafiti huu yaliyotokana na majibu ya mahojiano baina ya mtafiti na walimu wakuu wa shule tano za sekondari za wilaya ya Ilemela yanaonyesha kwamba elimu ya sekondari kutofundishwa kwa lugha ya Kiswahili athiri ubora wa elimu ya kiwango hicho. Kwa mfano, mkuu wa shule moja kati ya hizo alisisitiza kwa kusema kwamba:

“Mimi ninasikitika sana kuona elimu yetu inazidi kuporomoka sababu kubwa ni lugha ya kufundishia kutoeleweka kwa walimu na wanafunzi. Utakuta mwalimu anayefundisha somo la Jografia anatumia muda mwingi kufafanua somo hilo kwa kutumia lugha ya Kiswahili hapo wanafunzi watafurahi sana lakini akibadili kidogo na kufundisha kwa Kiingereza wanafunzi hao hao wanashindwa kuchangia lolote hatuwezi kuboresha elimu kwa kutumia lugha isiyoeleweka”

Mwalimu mkuu wa shule ya sekondari nyingine alihoji kwa kusema kwamba:

“Hivi ni kwanini serikali isiamue kutumia lugha innayoeleweka kwa wliowengi kufundishia elimu ya sekondari ili kunua viwango vya ufaulu?”

Hivyo basi, uchambuzi wa data hizo unaonyesha kuwa, suluhisho la kudumu ni kuhalalisha Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia elimu katika ngazi ya elimu ya sekondari nchini Tanzania. Kwa mujibu wa Vuzo (2002) lugha ya kufundishia inaweza kuathiri uwezo wa wanafunzi kufafanua maelekezo na maswali. Aidha, mwalimu na mwanafunzi wanaathiriana pale Kiswahili kinapo kuwa lugha ya kufundishia, na wanafunzi wengi wanakuwa wepesi kuelewa na kujibu maswali yanaulizwa katika lugha ya Kiswahili

Pia, walimu wa shule zote tano za sekondari wanaofundisha masomo yanayofundishwa kwa Kiingereza walikiri katika mahojiano kwamba, kuna ugumu wa kufundisha darasa la kidato cha kwanza. Wakati mwingine wanaogopa kupangiwa kidato cha kwanza. Walimu hao waliendelea kudai kwamba, wanapokuwa darasani kufundisha kidato hicho, wanafunzi wanawatatazama tu walimu, kuashiria kwamba hawaelewi. Pia walimu walikiri kuwa kutumia lugha mbili za Kiswahili na Kiingereza huwafanya wanafunzi waelewe kinachofundishwa kinyume na matakwa ya sera ya elimu Tanzania ya mwaka 2014. Hii ni dalili kwamba lugha ya

kufundishia elimu ya sekondari haifai tena. Ni dhahiri kwamba, mchakato wa usomaji na ujifunzaji utakuwa mgumu, na muda hautatosha kufundisha mada zote

Pia wanafunzi walengwa ambao walihojiwa, walikikri kwamba kuna athari nyingi zinazotokana na kutfundishwa kwa lugha ya Kiswahili. Wanafunzi hao walisema kwamba, wanamaliza elimu hiyo ya sekondari wakiwa hawana ujuzi wowote. Jambo hilo halitasaidia taifa kusonga mbele.

Kwa jumla, majibu yaliyopatikana kwa njia za mahojiano yanaendana na kushabihiana na majibu yaliyopatikana kwa njia ya dodoso ambayo yameonyesha kuwa na athari hasi kuliko chanya.

Uchambuzi wa data katika lengo la pili la utafiti unaonesha kwamba, kuna athari nyingi zitokanazo na kutotumia lugha ya kiswahili kufundishia elimu ya sekondari. Hivyo, inapendekezwa kwamba suluhisho la kudumu la athari hizo ni kuhalalisha Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia elimu katika ngazi ya elimu ya sekondari nchini na Kiingereza kifundishwe vizuri kama somo kwa ajili ya mawasiliano ya kimataifa.

4.4 Changamoto Zinazowakabili Walimu na Wanafunzi Kutokana na Kiswahili Kutotumika Kufundishia Elimu ya Sekondari

Mtafiti alitumia hojaji kwa njia ya maswali ya dodoso kuwauliza walimu kama kuna changamoto zinazowakabili walimu na wanafunzi kutokana na Kiswahili kutotumika kufundishia elimu ya sekondari. Matokeo kutokana na majibu ya swali dodoso hili

yalionyesha kuwa asilimia 76%(19) ya walimu waliyonyesha kwamba kuna changamoto zinazowakabili walimu na wanafunzi kutokana na Kiswahili kutotumika kufundishia elimu ya sekondari. Aidha, asilimia 16%(4) walikataa kwamba hakuna changamoto zinazowakabili walimu wakati 8%(2) ya walimu hawakuonyesha mwelekeo wowote kuhusu swali hili.

Jedwali 4.5: Majibu ya Walimu na Wanafunzi Kuhusu Changamoto Zinazowakabili Walimu Na Wanafunzi Kutokana Na Kiswahili Kutotumika Kufundishia Elimu ya Sekondari

A Maswali ya Dodoso kwa Waalimu					
Na.	Changamoto zinazowakabili walimu na kutokana na Kiswahili kutotumika kufundishia elimu ya sekondari	Majibu			
		Ndiyo	Hapana	Sijui	Jumla
		% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi
1	Walimu kutomaliza mada kwa wakati kutokana na kufundishia lugha mbili kwa wakati mmoja	76%(19)	16%(04)	8%(02)	100%
2	Ujuzi mdogo kwa lugha ya Kiingereza	60%(15)	32%(8)	8% (02)	100 %
3	Wanafunzi kutoelewa masomo haraka	73%(19)	27%(6)	0%(0)	100%
B Maswali ya Dodoso kwa Wanafunzi					
Na.	Changamoto zinazowakabili wanafunzi kutokana na Kiswahili kutotumika kufundishia elimu ya sekondari	Majibu			
		Ndiyo	Hapana	Sijui	Jumla
		% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi	% na Idadi
1	Wanafunzi kutoelewa vizuri masomo	95%(76)	3.75%(4)	1.25%(01)	100%
2	Wanafunzi kushindwa mitihani	85%(68)	16.25%(13)	1.25%(1)	100 %
3	Wanafunzi kukosa uwezo wa kujieleza, kusoma na kuandika kwa Kiingereza	90%(72)	7.5% (6)	2.5%(2)	100%

Chanzo: Utafiti wa uwandani: 2015

Mtafiti aliwauliza wanafunzi pia kama kutoeleweka kwa lugha ya Kiingereza katika shule kuna leta changamoto kwa walimu na wanafunzi wa sekondari. Matokeo

kutokana na majibu ya wanafunzi juu ya swali dodoso hili yanaonyesha kuwa asilimia 95%(76) ya wanafunzi wote 80 waliotakiwa kujibu swali hilo yanaonyesha kuwa kuna changamoto zinazowakabili walimu na wanafunzi zitokanazo na kutotumika kwa Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari. Aidha, asilimia 3.75%(3) walikataa kuwa hakuna changamoto wakati asilimia 1.25% (01) hawakuwa na mwelekeo wowote kuhusu swali hili. Jedwali namba 4.4 linadhihirisha haya matokeo.

Matokeo haya yanaashiria kwamba walimu 76% wanapata changamoto za kutotumika kwa lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari. Aidha, matokeo haya yanaashiria kwamba, kutotumika kwa Kiswahili kuna toa changamoto za walimu kushindwa kumaliza mada mapema na pia kutofikia malengo ya mtaala kwa wakati

Kwa upande wa wanafunzi, matokeo ya utafiti huu yanaashiria kuwa suala la changamoto zitokanazo na elimu ya sekondari kutofundishwa kwa Kiswahili, halizingatiwi katika ufundishaji wa elimu wilayani Ilemela. Kutokana na hali hiyo, wanafunzi wa sekondari katika wilaya hii hawapati maarifa ya kutosha ya kiwango cha elimu ya sekondari. Hii inadhihirishwa na majibu yalitolewa na wanafunzi 95% walikiri kwamba, wanafunzi wanapata changamoto nyingi za kutofundishwa kwa lugha ya Kiswahili wakati asilimia 3.75% walikanusha na asilimia 1.25 hawakuwa na mwelekeo.

Kwa mujibu wa Rubagumya (2003) anadai kwamba, lugha ya kufundishia katika elimu ya sekondari unaonyesha kwamba, mfumo wa elimu wa matumizi ya lugha mbili za kufundishia umewapa wanafunzi matokeo hasi. Kwa mtazamo wa mtaalamu

huyo ni wazi kwamba lugha ya kufundishia inapaswa kuwa lugha moja ambayo inaeleweka kwa ufasaha kwa walimu na wanafunzi ili kuwezesha wanafunzi kupata maarifa mapya yanayofundishwa kwa lugha wanayoielewa vizuri.

Matokeo ya utafiti huu yanaashiria kuwa, hoja hii haizingatiwi katika ufundishaji wa elimu ya sekondari wilayani Ilemela. Kutokana na hali hiyo, wanafunzi wa sekondari katika wilaya hii hawapati vema maarifa yanayokusudiwa kwa ajili yao. Hii inadhihirishwa na majibu yalitolewa na walimu kwamba, matumizi ya lugha ya kigeni una changamoto, si tu kwa wanafunzi bali pia kwa walimu. Changamoto kwa walimu ni pamoja na kutomaliza mada zao kwa wakati kutokana na vikwazo vya lugha, inayopunguza kasi yao ya ufundishaji. Lakini pia walimu wengi hawana uelewa wa kutosha wa lugha ya kigeni kwa kiwango cha kuifanya itumike kufundishia. Matokeo yake, walimu, kwa upande mmoja, hulazimika kutumia lugha mchanganyiko si tu kuwafanya wanafunzi wao waelewe vizuri, bali huwapa hata wao walimu urahisi wa kuwasilisha masomo yao. Tafsiri yake ni kwamba, kama mwalimu anapata ugumu wa kujieleza kwa lugha ya kigeni, na kumlazimu wakati mwingine kuchanganya lugha, ni dhahiri kwamba uwasilishaji wa somo lake si kamilifu kama atalazimika kutumia lugha ya kigeni.

Ugunduzi wa utafiti huu unashabahiana na ule wa Mwinsheikhe (2003) aliofanya, akitaka kujua kama kutumia Kiswahili katika mchakato wa kufundisha na kujifunza kunaweza kuimalisha ushiriki na ufaulu wa wanafunzi kwa masomo ya sayansi. Aligundua kwamba, kuna tatizo la lugha katika kufundisha sayansi. Walimu wengi walikiri kutumia lugha ya Kiswahili wanapofundisha masomo hayo kinyume

na sera ya elimu ya Sekondari.Hali hii haiwaendelezi wanafunzi na jamii nzima ya watanzania bali inarudisha juhudi za maendeleo ya nchi kwa jumla.

Naye Tikolo (2012) anatoa hoja kwamba, ufahamu wanafunzi kwa lugha aliyoizoea wakati wa kukua kwake inaweza kuwa ndiyo msingi wa ujifunzaji mzuri wa baadaye pale anapounganisha na ujuzi wa mwalimu wake.

Matokeo ya utafiti huu yanathahirisha kuwa hoja hii haizingatiwi katika ufundishaji wa elimu ya sekondari wilayani Ilemela.Kutokana na hali hiyo, wanafunzi wa sekondari katika wilaya hii hawapati vema maarifa yanayokusudiwa kwa ajili yao.Hii inabainishwa na majibu yalitolewa na wanafunzi kwamba, kutofundishwa kwa lugha ya Kiswahili ni changamoto kubwa. Miongoni mwa changamoto hizo ni wanafunzi kutoelewa vizuri somo wanalofundishwa, wanafunzi kushindwa mitihani, wanafunzi kuathirika na tamaduni za kigeni zinazoambatana na lugha hizo, wanafunzi kukosa uwezo wa kujieleza, kuandika na kusoma; ambavyo ndivyo ni mojawapo ya misingi ya kumfanya mwanafunzi ajiamini, afikiri sawa sawa na awe mbunifu katika usomaji na ujifunzaji.

Tafsiri ya ugunduzi huu ni kwamba, mpaka sasa, tafiti nyingi hazihusianishi moja kwa moja kushindwa kwa wanafunzi kama mojawapo ya athari ya matumizi ya lugha. Badala yake, lawama nyingi huelekezwa kwa walimu kutofundisha vizuri, huku ikisahaulika kwamba, hata walimu nao hupata vikwazo vya lugha ya kigeni katika kufundisha. Lakini pia, viongozi wengi wa serikali hawahusianishi moja kwa moja kwa changamoto za matumizi ya lugha ya kigeni kufundishia elimu na

kuporomoka kwa maadili, mila, desturi na tamaduni za kiafrika, hususani za kitanzania; Kinyume chache, lawama nyingi huelekezwa kwa wazazi na wanajamii kwa ujumla. Mpaka sasa tafiti nyingi hazihusianishi kwa kupungua kwa uwezo wa watanzania kung'amua na kufikiri sawasawa, kupungua kwa uwezo wa kubuni na kugundua kunachangiwa sana na matumizi ya lugha ya kigeni kufundishia elimu, na hasa elimu ya sekondari.

Haijulikani sababu za kigugumizi cha serikali kushindindwa kuamua kuwa Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia elimu ya sekondari wakati kikiwa na uwezo wa kubeba majukumu hayo ya kitaaluma. Kwa mujibu wa Msanjila na wenzake (2009) wanasema kwamba, uwezo wa Kiswahili kuingizwa kwenye teknolojia ya habari na mawasiliano kunawathibitisha wenye mamlaka kwamba Kiswahili kinauwezo wa kukabili hata mambo yasiyo asili yake. Pia kina nguvu ya kuwapa uwezo wa kutumia teknolojia hiyo kufanyia mambo yao na si yale tu yenye asili ya kigeni. Kwa mujibu wa Mwinsheikhe (2003) anahoji kwamba huo woga wa kuamua kutumia Kiswahili unatoka wapi, wakati Tanzania ilishapata kamusi ya mwongozo kwa masomo ya Biologia, Kemia na Fizikia tangu 1990 ambayo inaondoa woga kwa pale palipo kuwa na ugumu.

4.4.1 Mambo Yanayozuia Lugha ya Kiswahili Kufundishia Sekondari

Swali la tatu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza mambo yanayochangia Kiswahili kukosa hadhi ya kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari. Mtafiti alikusudia kufahamu toka kwa walimu kama yapo mambo yanayochangia kukwamisha lugha ya Kiswahili kupata hadhi ya kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari. Data za

swali hili zilikusanywa kwa kutumia dodoso kwa swali la tisa mpaka la kumi na moja. Lakini pia swali la tatu la mahojiano lililenga kupata data kwa ajili ya ulinganifu na data za dodoso ili kupata data zenye uhalisia na zenye tafsiri sahihi ya majibu ya mhojiwa.

4.4.2 Vikwazo vya Kiswahili kuwa Lugha ya Kufundishia Sekondari.

Walimu 25 sawa na asilimia mia moja (100%) walikubali kuwa kuna vizuizi ambavyo hufanya Kiswahili kisipate dhima ya kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari Tanzania. Vikwazo vikuu vilivyotajwa na wahojiwa ni kwamba: Viongozi wa serikali na siasa hawakipi umuhimu wa pekee kiswahili na kukipa jukumu la kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari. Kwa kupendelea lugha ya kigeni kwa kujificha kwenye mwamvuli wa utandawazi kwamba watanzania hawatakiwi kuishi kisiwa cha pekee yao. Vilevile kuna kudharaulika kwa lugha ya Kiswahili kwa walimu na wanasiasa wanao pendelea lugha ya kigeni hata kama hawawezi kuitumia kwa ufasaha.

Vizuizi vingine ni viongozi wengi wanakumbatia mfumo wa elimu inayotumia lugha ya kikoloni hata kama haina tija kwa taifa la sasa. Vitabu vingi vimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza hivyo si rahisi kuvitafsiri kwa lugha ya Kiswahili. Ukosefu wa vitabu vilivyokwisha wekwa katika mfumo wa lugha ya Kiswahili. Aidha, kuna misamiati migumu hasa ya kisayansi isiyozoeleka ni kikwazo kwa walimu na wanafunzi. Baadhi ya viongozi wa serikali na kisiasa wanamiliki shule za binafsi zenye kutumia lugha ya kigeni kufundishia, kwa hiyo, si rahisi kukubali kubadirisha mfumo wa lugha ya kufundishia, kwani kwao haina masilahi.

Hivyo, uchambuzi wa data unaonyesha kuwa lugha ya Kiswahili inakabiliwa na vikwazo vingi vinavyofanya kikose hadhi ya kuwa lugha ya kufundishia. Vikwazo hivyo vinawagusa zaidi viongozi wa serikali, wanasiasa na baadhi ya wanasiasa wanaomiliki shule za sekondari za binafsi zenye mfumo wa matumizi ya lugha za kigeni katika kufundishia elimu ya sekondari.

4.4.3 Majibu ya Mahojiano

Matokeo ya uchunguzi huu kwa njia ya maswali ya mahojiano yanaonyesha kuwa walimu walikubali kuwa kuna vikwazo vinavyozuia lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya kiswahili ya kufundishia elimu ya sekondari .

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa lugha ya Kiswahili inakabiliwa na vikwazo vingi. Hayo yanathibitishwa na majibu ya wanafunzi kwamba, Serikali haitaki kuamua kutumiwa kwa lugha ya kiswahili kuwa lugha ya kufundishia. Hili linasababishwa na ukweli kwamba, wao walisoma kwa lugha ya Kiingereza na wakafanikiwa, basi wanafikiri watu wote wanaweza kufanikiwa kwa kusoma kwa Kiingereza. Kwa hiyo, tatizo hapa ni viongozi kutokuamua kwa dhati juu ya hatima ya wanafunzi wa sekondari. Wao wanaiga kila kitu toka ulaya, kama vile hawaoni kwamba hao wanaoigwa hutumia lugha yao kujifunzia

Hali kadhalika, walimu walikubaliana na majibu ya wanafunzi kwa kusema,

Tatizo la viongozi waliosoma wakati wa ukoloni, Walirithi kila jambo la kikoloni, na wao wenyewe waliathirika na ukoloni. Waliendelea kuwa na fikra za kikoloni. Waliendelea kuthamini vya kikoloni kuliko vyetu. Waliendelea kurithisha mifumo ya

kikoloni ingawa ilirekebishwa kwa kuweka viraka ili ionekane ni ya Kitanzania. Ndiyo maana, mambo mengi walipingana na Hayati Mwalimu Nyerere kwa sababu alikuwa anachukia kwa dhati ukoloni na mambo yao (CHANZO CHAKO NI KIPI??). Kwamba huko zamani, ilikuwa mtu akijua kuzungumza Kiingereza alionekana msomi. Huko ni kukuza lugha ya kigeni kwa kuuu au kudumaza lugha yetu, bila wao wenyewe kujua.

Kwa hali hiyo, matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kuwa, lugha ya Kiswahili inakabiliwa na vikwazo vingi vinavyofanya kikose hadhi ya kuwa lugha ya kufundishia. Vikwazo hivyo vinawagusa zaidi viongozi wa serikali, wanasiasa na baadhi ya wanasiasa wanaomiliki shule za sekondari za binafsi zenye mfumo wa matumizi ya lugha za kigeni katika kufundishia elimu ya sekondari. Pia, vikwazo hivyo vinaambatana na athari za kurithi elimu ya kikoloni, lugha ya kikoloni pamoja na ukiritimba wa kifikra ya kutokukubali kwa dhati hadhi na thamani ya Kiswahili kuliko ilivyo kwa lugha ya Kiingereza.

4.4.4 Majumuisho ya Lengo la Tatu la Utafiti

Uchambuzi wa data kutokana na majibu ya dodoso pamoja na ya mahojiano yanaonesha kuwa lugha ya Kiswahili inakabiliwa na vikwazo vingi vinavyofanya kikose hadhi ya kuwa lugha ya kufundishia. Vikwazo hivyo vinawagusa zaidi viongozi wa serikali, wanasiasa na baadhi ya wanasiasa wanaomiliki shule za sekondari za binafsi zenye mfumo wa matumizi ya lugha za kigeni katika kufundishia elimu ya sekondari. Pia, vikwazo hivyo vinaambatana na athari za kurithi elimu ya kikoloni, lugha ya kikoloni pamoja na ukiritimba wa kifikra ya

kutokukubali kwa dhati hadhi na thamani ya Kiswahili kuliko ilivyo kwa lugha ya Kiingereza.

Utafiti huu ulibaini kuwa, ili kuwa na ufumbuzi wa kudumu kuhusu lugha ya kufundishia elimu ya sekondari inabidi; Serikali na wadau wote wa elimu waamue kwa dhati kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika shule za sekondari Tanzania na wasomi na wanasiasa waache kasumba ya kuthamini lugha ya kigeni isiyo na faida kwa wanafunzi wa sekondari nchini Tanzania.

4.5 Hitimisho

Kwa jumla utafiti huu umegundua kwamba, walimu na wanafunzi wanapendelea elimu ya sekondari itolewe kwa lugha ya Kiswahili badala ya kutumia lugha ya kigeni. Walimu na wanafunzi hao ndio wanaopata ugumu wa kutumia lugha hiyo, basi ni dhahiri kuwa utolewaji wa elimu ya sekondari kwa lugha ya kigeni hauna mafanikio makubwa hata kama kauli mbiu ya sasa ya serikali ni matokeo makubwa sasa. Ni vigumu kupata matokeo makubwa ikiwa wanafunzi hawaelewa wanachofundishwa. Ili kupata matokeo makubwa na yenye ufanisi ni lazima serikali na wadau wote wa elimu waamue kukifanya kiswahili kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari.

Sababu zinazotolewa hazina tija kwa mstakabali wa jamii ya watanzania kwa sasa, nyingi ya hizo nin kwa faida ya viongozi tu na si jamii nzima. Zipo sababu nyingi zinazosemwa katika kuthibitisha umuhimu wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia elimu ya sekondari. Mojawapo ya sababu hizo ni kwamba,

Kiswahili ni lugha ya kwanza kwa baadhi ya watanzania na ya pili kwa wengine, ambayo mtoto hukua nayo. Lakini pia, Kiswahili ndiyo lugha ya kufundishia elimu ya awali na ya msingi.

SURA YA TANO

5.0. MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii ni sura ya mwisho ambayo inawasilisha na kujadili muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu kuhusu haja ya lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia elimu ya sekondari. Sehemu ya kwanza ya sura hii inahusu muhtasari, sehemu ya pili ni hitimisho na sehemu ya tatu ni mapendekezo.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulikusudia kuchunguza kama kuna haja ya lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia elimu ya sekondari kwa kutumia mfano wa shule za sekondari za manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza. Walimu wa shule za sekondari wanaweza kufundisha kwa kujiamini na kwa ufanisi kama watatumia lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari hivyo wanafunzi kuyapata na kuyaelewa vema maarifa ya elimu ya kiwango hicho cha elimu. Walimu wengi wamekiri kuwa wanapata ugumu sana wa kufundisha kwa ufanisi na kueleweka kwa wanafunzi wao kwa sababu hawana umilisi wa kutosha wa lugha ya kigeni kwahiyo wangefundisha elimu ya sekondari kwa ufanisi kama wangetumia lugha ya Kiswahili.

Aidha, wanafunzi wengi wamekiri kuwa wanashindwa kupata maarifa kwa sababu hawaelewi vema lugha inayotumika kufundishia elimu ya sekondari. Ili kupata chimbuko la tatizo hili utafiti huu umejikita zaidi kuchunguza mambo mbalimbali ambayo yamechangia wanafunzi kukosa maarifa ya elimu ya sekondari, athari zitokanazo na kutotumika kwa lugha ya Kiswahili katika kufundishia elimu ya

sekondari na changamoto zinazo wakabili walimu na wanafunzi zitokanazo na kutotumika kwa Kiswahili katika ufundishaji wa elimu ya Sekondari.

Matokeo ya utafiti huu yalikusudiwa kutoa taarifa ambazo zingesaidia kuinua ubora wa ufundishaji wa elimu ya sekondari kitaaluma ili wanafunzi wapate maarifa ya kutosha wamalizapo elimu ya sekondari. Utafiti huu pia ulitarajiwa uwawezeshe wakuza mitaala kupitia upya mitaala ya elimu ya sekondari na kuyaweka maarifa yote katika lugha ya Kiswahili. Aidha, ilitarajiwa kuwa utafiti huu uwashawishi watunga sera, serikali na maafisa wanaofanya maamuzi katika wizara ya elimu na mafunzo kuonyesha utashi wa dhati kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundisha elimu ya sekondari. Mwisho matokeo ya utafiti huu yalitarajiwa kuwa msingi wa tafiti zingine juu ya suala hili. Maswali ya utafiti yalioongoza utafiti huu ni; Kwa nini hadi leo Kiswahili hakitumiki kufundishia elimu ya sekondari Tanzania? Je nini athari zinazotokana na kutotumika lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari? Ni changamoto gani zinazowakabili walimu na wanafunzi kwa kutotumika kwa Kiswahili katika ufundishaji wa elimu ya sekondari?

Data zilikusanywa kwa mbinu za hojaji, mahojiano na utafiti wa maktabani. Uchambuzi wa data ulifanyika na matokeo kuwasilishwa kwa njia ya maelezo na majedwali katika asilimia na idadi. Utafiti ulifanyika katika shule za sekondari za serikali tu. Utafiti huu ulihusisha sampuli ya walimu wa darasani wa masomo mbalimbali 20, wanafunzi 80 na wakuu wa shule za sekondari tano (05). Utafiti umethibisha kuwa kuna haja kubwa sana ya lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia elimu ya sekondari.

5.3 Hitimisho

Utafiti huu umeshughulika na vipengele muhimu vya lugha ya kufundishia elimu ya sekondari katika eneo la utafiti. Kwa mujibu wa maswali ya utafiti yanayohusika na utafiti huu, hitimisho na mapendekezo yafuatayo yanatolewa.

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza *Haja ya lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia elimu ya Sekondari: Mifano kutoka wilaya ya Ilemela-Mwanza*. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza uhusiano baina ya kutotumika kwa Kiswahili katika ufundishaji wa masomo katika shule za sekondari na kushindwa kwa wanafunzi kupata maarifa yaliyokusudiwa. Malengo mahususi ya utafiti huu yalikuwa ni; Kubaini mambo yanayo changia wanafunzi kukosa maarifa ya elimu ya sekondari, kutathimini athari zitokanazo na kutokutumika kwa lugha ya Kiswahili katika kufundishia elimu ya sekondari na kubaini changamoto zinazowakabili walimu na wanafunzi zitokanazo na kutotumika kwa Kiswahili katika ufundishaji wa elimu ya sekondari.

Kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu, matokeo ya utafiti yamethibisha kwamba, ipo haja ya elimu ya sekondari kufundishwa kwa lugha ya Kiswahili. Sababu kubwa ni kwamba, lugha ya Kiswahili ndiyo lugha ya mawasiliano mapana ya Watanzania walio wengi kwa sababu lugha hii hivi sasa ni lugha ya kwanza. Lugha hii imezoeleka na inafahamika vizuri kwa walimu na wanafunzi walio wengi kwa kuzungumza na kuandika. Aidha, lugha ya Kiswahili tayari hutumika mara kwa mara kwa mawasiliano kati ya wanafunzi na walimu, na baina ya wanafunzi wenyewe na wazazi nyumbani. Si hayo tu lakini pia lugha ya Kiswahili imeshakua kwa kiwango

cha kutumika katika nchi nyingine nyingi. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kuwa, mambo yanayochangia kwa kuzingatia wanafunzi kukosa maarifa ya elimu ya sekondari ni; Kiswahili kutotumika kufundishia elimu ya sekondari, kutoeleweka vizuri lugha ya Kiingereza katika shule za sekondari, Kiswahili kutopewa umuhimu wa kutumika kufundishia elimu ya sekondari. Mbinu zilizobainika kuwa zinastahili kuondoa tatizo la wanafunzi kukosa maarifa ya elimu ya sekondari ni; Kiswahili kupewa dhima ya kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari, Kiswahili kipewe umuhimu wa kutumika kufundishia elimu ya sekondari, Kuwepo na mikakati ya dhati ya kutafsiri vitabu na machapisho katika lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu pia ulichunguza athari zitokanazo na kutokutumika kwa lugha ya Kiswahili katika kufundishia elimu ya sekondari. Matokeo yalionesha kuwa athari hizo ni; Kushuka ubora wa elimu kitaaluma, wanafunzi kushindwa kutumia uwezo na ujuzi wa kubuni na kung'amua mambo yanayowakabili baada ya kumaliza elimu ya sekondari, vikwazo vya mawasiliano baina ya walimu na wanafunzi, mwalimu kutumia lugha zaidi ya moja darasani, mada kutokwisha kwa wakati na somo kutoeleweka kwa urahisi, wanafunzi kukosa uwezo wa kujibu vizuri maswali ya kujieleza na kutoshiriki kujibu maswali darasani, wanafunzi kushindwa kumudu taaluma, wanafunzi kushindwa kufaulu mitihani kwa viwango stahiki, wanafunzi kupewa adhabu za kuongea Kiswahili shuleni.

Aidha, utafiti huu umejadili kuwa, ufumbuzi wa athari zitokanazo na kutokutumika kwa lugha ya Kiswahili katika kufundishia elimu ya sekondari ni; Kiswahili kipewe kipaumbele kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari ili kuwapa urahisi walimu

na wanafunzi kuwasiliana na kuelewa masomo ya sekondari na lugha ya Kiingereza ifundishwe kama somo kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi kuwa na ufahamu wa kuwasiliana kimataifa.

Utafiti huu ulichunguza changamoto zinazowakabili walimu na wanafunzi kutokana na Kiswahili kutotumika kufundishia elimu ya sekondari. Katika utafiti huu changamoto zilizobainika ni pamoja na; walimu kutomaliza mada kwa wakati kutokana na kufundishia lugha mbili kwa wakati mmoja, walimu wana ujuzi mdogo wa kutumia lugha ya Kiingereza, wanafunzi kutoelewa masomo haraka, wanafunzi kushindwa mitihani, wanafunzi kukosa uwezo wa kujieleza, kusoma na kuandika kwa Kiingereza.

Aidha, ili kutatua changamoto hizo utafiti huu ulibaini kuwa; Serikali na wadau wote wa elimu waamue kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika shule za sekondari na wasomi na wanasiasa waache kasumba ya kuthamini lugha ya kigeni isiyo na faida kwa wanafunzi wa sekondari nchini Tanzania.

5.4 Mapendekezo

5.4.1 Mapendekezo ya Jumla

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, inapendekezwa kwamba; Serikali ione uwezekano wa kuipa hadhi lugha ya Kiswahili na kuirasmisha kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari kwa lengo la kukuza viwango vya ufahamu na ufaulu, uchumi, kuendeleza utamaduni wa taifa na kuimarisha lugha ya Kiswahili. Vile vile, serikali kupitia wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi ione uwezekano wa

kulifanya Somo la Kiingereza kuwa somo la lazima kwa viwango vyote vya elimu ili kuimarisha ufahamu wa mawasiliano ya lugha ya kimataifa, sambamba na mafunzo kwa walimu wa somo hilo ili kuwajengea uwezo wa kumudu kutumia na kufundisha. Pia watunga sera wafanye utafiti kwa kuzingatia mazingira ya sasa, na kwa kutunia wataalamu waliobobea katika tafiti za lugha za kufundishia, juu ya uhalali wa kuendelea kutumia lugha ya kigeni kufundishia elimu ya sekondari Tanzania, na kisha hatua stahiki zichukuliwe kuhusu lugha ya kufundishia katika mifumo ya elimu Tanzania.

5.4.2 Mapendekeo kwa Tafiti Zijazo

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza uhusiano baina ya kutotumika kwa Kiswahili katika ufundishaji wa masomo katika shule za sekondari na kushindwa kwa wanafunzi kupata maarifa yaliyokusudiwa katika manispaa ya Ilemela jijini Mwanza. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, utafiti huu unapendekeza kuwa; Utafiti kama huu ufanyike zaidi katika maeneo mengine zaidi ya manispaa ya Ilemela ili kuchunguza kama haya matatizo yanayowakabili walimu na wanafunzi wa manispaa hii pia yako huko. Ufanyike utafiti kuhusu sera ya elimu juu ya lugha ya kufundishia elimu ya sekondari nchini ili iweze kukidhi mahitaji ya Watanzania kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa maarifa ya kutosha na endelevu ya elimu ya sekondari nchini Tanzania.

MAREJEO

- August, D. na Shanahan, T. (Eds.), (2006). *Developing Literacy in Second-language Learners*, Mahwah, NJ: Erlbaum.
- Batibo, H. M. (1995). *The Growth of Kiswahili as Language of Education and Administration in Tanzania*. In putz, Martin (ed.). *Discrimination through language in Africa. Perspectives on the Namibian experience*. Berlin: Mouton de Gruyter
- Bostwick, R. M. (1999). *A study of an elementary English language immersion school in Japan*. Unpublished Doctoral dissertation, Temple University, Philadelphia
- Brock-Utne na wenzake (eds), (2003). *Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA)*. Dar es Salaam: E& D publishers
- Brock-Utne, B. (2005). *Language-in- Education policies and practices in Africa with a special focus on Tanzania and South Africa*. in. A.M.Y Lin na P.W.Martin (ed, *Decolonization, Globalisation. Language –in- Education policy and practice*. Buffalo: Multilingual Matters Ltd.
- Brock-Utne, B.(2005). *Learning through a familiar language versus learning through a foreign language. A look into some secondary school classroom in Tanzania*. Paper presented at the LOITASA work shop at the University of Western Cape, Cape Town 25 April 2005.
- Brock-Utne, B na wenzake (2005). *LOITASA Research in progress. Language of Instruction in Tanzania and South Africa*. Dar es Salaam: KAD Associates.
- Brock-Utne, B. (2000). *Whose Education for All? Re-colonization of the African mind*. New York: Falmer press

- Brock-Utne, B. (2002). Language, Democracy and Education in Africa. Discussion paper no. 15. Uppsala. Nordic Africa Institute Available from the nai website.
- Brock-Utne, B. (2003). Language Question in Africa in the light of Globalisation, social justice and Democracy International Journal of peace studies, vol.8.no.2
- Bryman A. (2008). Social Research Methods. London. Oxford University Press
- Cummins, J. (2008). Teaching for transfer. Challenging the two solitudes assumption in Bilingual education. In J. Cummins & N.H Homberger (Eds), Encyclopedia of Language and Education, 2nd Edition, Volume 5. New York: Springer Science + Business Media LLC.
- Enon C.J. (1995). Educational Research, Statistics and Measurement. Kampala: Makerere University.
- Infante, D. A., Rancer, A.S., & Womack, D. F. (1997) Building communication theory Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1982) Mfumo wa Elimu ya Tanzania 1981 – 2000.
- Ripoti ya Mapendekezo ya Tume ya Rais ya Elimu Juzuu I. Dar es Salaam.
- Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2011) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Sera ya Elimu ya Elimu na Mafunzo 2010
- Johnson, R. K. & Swain, M. (1997). Immersion education. International perspectives. Cambridge, UK: Cambridge University Press.
- Kaduma, Ibrahim: Opening Address to the LOITASA workshop, Arusha on 26th January, 2004.

- Kamugisha, D. J. na Mateng'e, F. J. (2004). Politics of curriculum making: A quandary to quality education in Tanzania? *International Journal of social science and Entrepreneurship* 1(9).
- Kaplan, R. na Baldauf, R. (1997) *Language planning from practice to theory*. Clevedon: Multilingual matters
- Kamwendo, Gr. H. (2000). Malawi's Approach to Language in Education: A Review of Key Issues." In *Language and Development in Southern Africa: Making the Right Choices*, ed. Richard Trewby and Sandra Fitchat, 86-93. Namibia: Gamsberg Macmillan Publishers.
- Kothari R. (2012). *Research methodology Methods and Techniques (Second Revised Edition)*. New Delhi: New age International Publishers.
- Kothari, C. R. (2004) *Research methodology Methods and Technique (Second Revised Edition)*. New Delhi: New age International Publishers
- Koul L. (2009). *Methodology of Educational Research, fourth Revised and Enlarge Edition*.
Inda Vikas publishing House PVT Ltd: New Delhi India.
- Lambert, W. Ena wenzie (1960) "Evaluational Reactions to Spoken Languages." *Journal of Abnormal and Social Psychology*. 20.1
- Lambert, W. E. (1984). An overview of issues in immersion education. In California State Department of Education (Ed.), *Studies on immersion education: A collection for United States educators*. Sacramento: California State Department of Education.

- Lockhart, L. (1985). Botswana: System of Education. In *The International Encyclopedia of Education*, ed. Torsten Husen and T. Neville Postlethwaite, 504-508. New York: Pergamon Press.
- Lwaitama, A. F. (2004). *The Kiswahili Language and Cultural Foundations of unity in Tanzania: Past and Present perspective*. Paper presented at a Joint ACCORD/MNF National Dialogue on Constitutional Development in Tanzania, Hotel Tulip, Dar es Salaam, 10th -14th December.
- Malekela, G. (2003) *English as a medium of Instruction in post-Primary Education in Tanzania*.
- Is it a Fair policy to the Learner? In Brigit Brock-Utne, Zubeida Desai, and Martha Qorro (eds) *Language of Instruction in Tanzania and South Africa*. Dar es Salaam: E& D Limited
- Malekela, G. (2004) *Secondary School Student's Views on the Medium of Instruction in Tanzania*. Paper presented at the LOITASA Workshop 26-28 January 2004. Arusha, Tanzania.
- Masato, M. (2004). *Kiswahili strategies to meet demand for language* Daily New. Saturday 30 October. p.2
- Massamba D.P.B. (2004) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya lugha*. Chuo kikuu cha Dar es Salaam. TUKI.
- May, S. H. R. (2008). *Bilingual/Immersion education. What the research tell us*. In J. Cummins & N.H. Homberger (eds.). *Encyclopedia of language and Education*, 2nd Edition, volume 5: *Bilingual Education*. New York: Springer science + Business + Business Media LLC.

- May, S. H. R and Tiakiwai,S.(2003,December).Bilingual Immersion education:Indicators of good practice.Final Report for New Zealand ministry of Education,Hamilton.Wilf Malcom Institute of Educational Research.
- Mekacha, R. (2000). Isimu jamii-Nadharia na muktadha wa Kiswahili. Osaka.?
- Mekacha, R. D. K. (1997). Language as a Determinant of the Quality of Education. A Rejoinder, Journal of Linguistics and Language in Education Vol 3:95-105.
- Department of Foreign Languages and Linguistics:University of Dar es Salaam.
- Mekacha.R.D.K (1995).Kwanini Kiingereza bado ni lugha ya kufundishia elimu ya juu Tanzania. (?):Kioo cha lugha
- Mkwizu, M. (2002).The pedagogical implications of Using English as the Medium of Instruction in Teaching Civics in Tanzania Secondary Schools,Paper presented at the LOITASA Workshp,26-28 January 2004.Arusha.Tanzania
- Mlama, P. na Matheru, M. (1980). Haja ya kutumia Kiswahili kama Lugha ya Kufundishia Katika Elimu ya Juu. Lugha Yetu 35 na 36. Dar es Salaam, BAKITA.
- MligoS.E (2012) Jifunze utafiti: mwongozo kuhusu utafiti na uandishi wa ripoti yenye mantiki. Dar es Salaam.Ecumenical Gathering (EGYS).
- Mochiwa,Z.(1991)Bifoculism or Unifoculism in education? A CRITICAL evaluation of Language policy in Tanzania. In John Hutchison na wenzake (eds) Issues in Language and Education.Boston.African Studies Centre
- Mochiwa, Z. S. M. (1979).The Impact of Kiswahili on ethnics languages.A case study of Handeni district.Unplished MA thesis:University of Dar es Salaam.

- MoEC (Ministry of Education and Culture),(1997) Sera ya Utamaduni. Dar es Salaam.
- Molosiwa, A. na wenzake (1991).A Comprehension Report on the Use of Setswana at all levels of Botswana's Education System.International Review of Education 37.
- Mpemba, T. (2007) Tanzania policy makers'Reluctance to Sanction Kiswahili Instructional medium in post –primary Education. How Do Learners and Instructors cope with or Resist the English medium policy? Dar es Salaam. University of Dar es Salaam (Tasnifu siyo chapishwa M. A).
- Msanjila, Y. P. (1990) Problems of Teaching through the Medium of Kiswahili ni Teacher Training Colleges in Tanzania. Journal of Multilingual and Multicultural Development II.
- Msanjila, P.Y na wenzake (2009) Isimujamii Sekondari na vyuo.Dar es Salaam.TUKI.
- Msanjila, P. Y. na wenzake (2000) Isimujamii Sekondari na vyuo.Dar es Salaam.Taasisi ya Uchunguzi Kiswahili
- Msanjila, P. Y na wenzake (2011) Isimujamii Sekondari na vyuo.Dar es Salaam. TUKI.
- Msanjila, Y. P. (2004). Kiswahili kitumike kufundishia shule za sekondari na Elimu ya juu Tanzania.In.Y.M Kihore and A. R. Chuwa (eds.), Kiswahili katika karne ya Ishirini na moja.Dar es Salam.TUKI:Chuo kikuu cha Dar es Salaam.
- Mwinsheikhe, H.(2003).Using Kiswahili as a Medium of Instruction in Science Teaching in Tanzania Secondary Schoos.in Birgit Brock-Utne,Zubeida

Desai and Martha Qorro (eds) Language of Instruction in Tanzania and South Africa. E&D Limited

Zhou, M. and Sun, H. (2004). Language Policy in the People's Republic of China: Theory and Practice Since 1948 [<http://www.utwente.nl/cw/theorieenoverzicht/theory>] kutembelea 2/1/2015 saa 9:00 mchana].

O-saki, K. M. (2003). Evaluation of lead Teacher Training Institutes in Ethiopia. A consultancy report prepared for UNESCO. Paris: UNESCO

Peterson, R. (2006). The use of an African language as language of Instruction at University level. The example of Kiswahili department at the University of Dar es Salaam in Tanzania. Oslo: Institute of Educational Research.

Puja, G. K. (2003). Kiswahili and Higher Education in Tanzania. Reflections Based on a sociological study from three Tanzanian university Campuses. In Brock-Utne, Birgit, Zubeida Desai and Martha Qorro (eds) (2003). The language of Instruction in Tanzania and south Africa (LOITASA). Dar es Salaam: E&D Publishers

Prah, K. 2005. Language and Instruction for Education, Development and African Emancipation. In Birgit Brock-Utne & Rodney Kofi Hopson (wah.). Languages of Instruction for African Emancipation. Cape Town: CASAS, Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Prah, K. (2003) Going Native: Language of Instruction for Education, Development and African Emancipation. Ktk.: Birgit Brock-Utne, Zubeida Desai na Martha Qorro (wah.). Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA). Dar es Salaam: E & D Publishers.

- Qorro M. A. S. (2006). Does language of Instruction Affect Quality of Education? University of Dar es Salaam, HakiElimu working Papers. Dar es Salaam
- Qorro M. A.S. (2003). Unlocking Language Forts. in *The Language of Instruction in post Primary Education in Africa with Special Reference to Tanzania*. in Birgit Brock-Utne, Zubeida Desai and Martha Qorro (eds) *Language of Instruction in Tanzania and South Africa*. E&D Limited.
- Qorro, M. A. S. (2005). Parents' Views on the Medium of Instructions in post-Primary Education in Tanzania. In: B. Brock-Utne na wenzake (eds) *LOITASA Research in progress*. Dar es Salaam. KAD Associates.
- Roy-Campbell, Z. M and Qorro, M. A. S. (1997). *Language Crisis in Tanzania. The Myth of English Vrsus Education*. Dar es Salaam. Mkuki na Nyota.
- Rubanza, Y. I. (2002). Realistic Revolutionary strategies in Harmonisation and Standardisation of African Languages'. In, Kwes Kwaa prah (eds.) *Rehabilitating African Languages*. The centre for advanced studies of African society. Cape Town
- Rubanza, Y. L. (1979). *The relationship between Kiswahili and other African languages. The case of kihaya*. Unpublished MA. thesis
- Rubanza Y. L. (1996). *Can a Three-Tier Language policy work in Tanzania? A new perspective*. A paper presented at the UCLA African Studies Centre. Dar es Salaam: Noon Seminar Series.
- Rubagumya, C. M. (1990). *Language in Tanzania*. In Casmir Rubagumya (ed). *Language in Education in Africa*. England. Multilingual matters Limited
- Rubagumya, C.M (2003). *English Medium Primary Schools in Tanzania. Anew Linguistic Market in Education?* in Birgit Brock-Utne, Zubeida Desai and

- Marth Qorro (eds)Language of Instruction in Tanzania and South Africa.E&D Limited
- Rugemalira, J. M. (2005). Theoretical and Practical Challenges in a Tanzanian English Medium School. Africa and Asia
- Senkoro, F. (2004). The role of language in education and poverty alleviation: Tool for access and empowerment in Justian Galabawa and Anders Narman Education poverty and Inequality (eds.Dar es Salaam.KAD Associates
- Skutnabb-Kangas, T. & McCarty, T. L. (2008). Key concepts in bilingual education: Ideological, historical, epistemological and empirical foundations. In J. Cummins and N. H. Hornberger (Eds.), Encyclopedia of Language and Education, 2nd Edition, Volume 5: Bilingual Education. New York: Springer Science + Business Media LLC.
- Swilla, I. N. (2009). Language of Instruction in Tanzania.Contradictions between Ideology, policy and Implementation. African study Monographs30 (1)
- TATAKI (2013). Kamusi ya Kiswahili sanifu Toleo la 3.Dar es Salaam: Oxford University press.
- Tibategeza, E. R. (2009). Language-in Education Planning in Tanzania: Sociolinguistic Analysis. Bloemfontein. University of the Free state (Tasnifu isiyochapishwa PhD)
- Tikolo, O. (2012).English Language In competency amongst Senior secondary school Graduates in Nigeria A-801: Education policy Analysis and Research utilization in comparative perspective, Harvard Graduate School of Education, December 12,201.
- TUKI (2010).Kamusi ya Kiswahili Sanifu.Dar es Salaam: Oxford University Press

Vuzo, M.S. (2002).Pedagogical Implications of using English s a language of instruction in secondary schools in Tanzania.Report,No.9.Education in Africa.Vol.11 also:Institute for Educational Research.

VIAMBATISHO

KIAMBATANISHO I: DODOSO LA WALIMU

TAARIFA TANGULIZI

1. Jina La Shule.....
2. Kata ilipo shule.....
3. Wilaya ilipo shule.....
4. Mkoa ilipo shule.....
5. Jinsi: Me () Ke ()

1. Je unadhani ipo haja ya kutumia lugha ya kiswahili kwa kufundishia elimu ya sekondari Tanzania? NDIYO () HAPANA ()
2. Je unadhani upo umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili katika kufundisha elimu ya sekondari ? NDIYO () HAPANA ()
3. Je ni lugha ipi inayoeleweka vizuri zaidi kwa mawasiliano baina ya wanafunzi na walimu wao na baina ya wanafunzi wenyewe?Taja.....
4. Unafikiri ni kwanini lugha hiyo inaeleweka vizuri zaidi kwa wanafunzi unaowafundisha ? Toa sababu
.....
5. Je unadhani zipo athari zozote za kutumia lugha ya kiswahili katika kufundishia elimu ya sekondari? NDIYO () HAPANA ()
6. Kama jibu lako ni NDIYO katika swali la (5) taja athari hizo;
.....

7. Yapi kati ya mambo yafuatayo yanaweza kuwa ni miongoni mwa athari zitokazo na kufundishia lugha ya Kiswahili kwa elimu ya sekondari nchini? Weka alama ya vema kwenye jambo unalodhani ni athari ya kutumia lugha ya kigeni katika kufundishia.
- Vikwazo vya mawasiliano dhidi ya walimu na wanafunzi ()
 - Matumizi ya lugha zaidi ya moja wakati wa kufundisha(kubadili msimbo) ()
 - Walimu wengi kupata changamoto katika kutumia lugha ya kigeni ()
 - Mada mbalimbali kutokwisha kwa wakati ()
 - Somo kutoeleweka kwa urahisi ()
 - Wanafunzi kutoshiriki vizuri katika kujibu maswali darasani ()
 - Wanafunzi kukosa uwezo wa kujibu vizuri maswali ya kujieleza ()
8. Nini ufumbuzi wa athari ulizobainisha katika swali la (5) na la (6) na la (7)? Eleza;
9. Je una udhani kuna changamoto zozote zinazo mkabili mwalimu na mwanafunzi zitokanazo na kutotumika kwa Kiswahili katika kufundishia elimu ya sekondari?NDIYO() HAPANA() Kama jibu ni ndiyo zitaje.....
10. Unadhani kuna mambo yoyote yanayokwamisha Kiswahili kisipewe dhima ya kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari Tanzania? NDIYO () HAPANA ()
11. Kama jibu lako ni Ndiyo katika swali (9) hapo juu,taja mambo hayo:-
.....
12. Kama jibu lako ni HAPANA katika swali la (9) hapo juu toa sababu
.....

KIAMBATANISHO II: DODOSO LA WANAFUNZI**TAARIFA TANGULIZI**

1. Jina la shule.....
2. Kata ilipo shule.....
3. Wilaya ilipo shule.....
4. Mkoa ilipo shule.....
5. Kidato.....
6. Jinsi: Me () Ke ()

1. Je, unadhani lugha gani ingefaa zaidi kutumika kufundishiwa elimu ya sekondari ?

2. Je, kuna athari zozote zinazotokana na kutofundishwa kwa lugha ya Kiswahili katika elimu ya sekondari? NDIYO () HAPANA ()

3. Kama jibu lako ni NDIYO katika swali la (3) hapo juu, taja athari hizo

Yapi kati ya mambo yafuatayo yanaweza kuwa ni baadhi ya athari za kutotumwa lugha ya kiswahili katika mchakato wa elimu ya sekondari? Weka alama ya vema kwenye jambo unalodhani ni athari za kutumia lugha ya kigeni katika kufundishia elimu ya sekondari.

- Kukaa kimya bila kuchangia mada za masomo darasani ()
- Kupewa adhabu kwa kuzungumza Kiswahili shuleni ()
- Kushindwa kujibu kwa ufasaha maswali ya darasani na maswali ya insha ()
- kushindwa kushiriki ipasavyo katika usomaji na ujifunzaji ()

- Woga wa kujieleza kwa kutumia lugha ya kigeni miongoni mwa wanafunzi ()

4. Je, ni nini kifanyike ili kutatua athari hizo? Eleza
.....
.....

5. Je una udhani kuna changamoto zozote zinazo mkabili mwalimu na mwanafunzi zitokanazo na kutotumika kwa Kiswahili katika kufundishia elimu ya sekondari?NDIYO () HAPANA() Kama jibu ni ndiyo zitaje.....
.....

Je,unadhani upo umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia elimu ya sekondari? NDIYO () HAPANA ()

6. Kama jibu lako ni NDIYO katika swali (7) hapo juu toa sababu;
.....

MASWALI ELEKEZI YA MAHOJIANO

KIAMBATISHO III: Maswali elekezi ya mahojiano ya walimu, wakuu wa shule

1. Je unadhani ipo haja ya kutumia lugha ya Kiswahili kwa kufundishia elimu ya sekondari Tanzania?
2. Nini athari zitokanazo kwa kutotumia lugha ya kiswahili katika kufundishia elimu ya Sekondari nchini?
3. Kwa nini Kiswahili bado hakijakubalika kufundishia masomo yote katika shule za sekondari hapa nchini Tanzania?

KIAMBATANISHO IV: Maswali elekezi ya mahojiano ya wanafunzi

1. Je unadhani ni lugha gani ingefaa zaidi kufundishia elimu ya sekondari?
2. Je unadhani upo umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari?
3. Je ni mambao gani yanayozuia Kiswahili kutopewa dhima ya kufundishia sekondari?